

**HOTUBA YA WAZIRI WA USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI, MHESHIMIWA DKT.
HARRISON G. MWAKYEMBE (MB),
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA KWA
MWAKA WA FEDHA 2015/2016**



“Mafanikio ya mtangamano wetu yanatutegemea sisi sote: viongozi, mataifa na kwa umuhimu mkubwa kabisa wananchi ambao ndiyo lengo kuu la kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.”

Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tarehe 20 Februari, 2015, Nairobi, Kenya.

VIONGOZI WA WIZARA



Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb)
WAZIRI



Mhe. Dkt. Abdulla J. Saadalla (Mb)
NAIBU WAZIRI



Bi. Joyce K.G. Mapunjo
KATIBU MKUU



Bw. Amantius C. Msole
NAIBU KATIBU MKUU

YALIYOMO	UK
YALIYOMO	i
VIAMBATISHO VILIVYO KATIKA HOTUBA	ii
1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2014/2015	5
3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO NA MPANGO WA MWAKA 2014/2015.....	12
3.1 SERA NA MIKAKATI	12
3.2 UTEKELEZAJI WA HATUA ZA MTANGAMANO	14
3.3 USHIRIKIANO NA KANDA NYINGINE ZA KIUCHUMI.....	27
3.4 USHIRIKIANO KATIKA SEKTA ZA UZALISHAJI.....	33
3.5 UENDELEZAJI WA MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI	37
3.6 USHIRIKIANO KATIKA SEKTA ZA HUDUMA ZA JAMII.....	46
3.7 USHIRIKIANO KATIKA SIASA, ULINZI NA USALAMA	53
3.8 BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI	61
3.9 MAHAKAMA YA AFRIKA MASHARIKI.....	63
3.10 ELIMU KWA UMMA	64
3.11 KUIMARISHA UWEZO WA WIZARA KIUTENDAJI	69
3.12 USIMAMIZI WA MAPATO NA MATUMIZI.....	72
4.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA.....	73
5.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/2016	76
6.0 SHUKRANI	80
7.0 MAOMBI YA FEDHA ZA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016.....	81

VIAMBATISHO VILIVYO KATIKA HOTUBA

1. KIAMBATISHO NA. 1: Bidhaa Ambazo Zimeingizwa Katika Mfumo wa Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki Katika Kipindi cha Majaribio.
2. KIAMBATISHO NA. 2: Mwenendo wa Biashara ya Jumla (*Total Trade*), 2007-2013 (US\$ Millioni).
3. KIAMBATISHO NA. 3: Miradi Iliyowekezwa Hapa Nchini na Nchi Wanachama Mwaka 2014.
4. KIAMBATISHO NA. 4: Mtandao wa Barabara wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
5. KIAMBATISHO NA. 5: Hatua iliyofikiwa ya Ujenzi wa Vituo Vya Utoaji wa Huduma kwa Pamoja Mipakani (*One Stop Border Posts-OSBPs*).

6. KIAMBATISHO NA. 6: Miswada ya Sheria Iliyopitishwa, Inayoendelea Kujadiliwa na Maazimio ya Bunge la Afrika Mashariki Katika Mwaka 2014/2015.
7. KIAMBATISHO NA. 7: Orodha ya Mashauri Yaliyosikilizwa na Kutolewa. Uamuzi katika Mwaka 2014/2015.
8. KIAMBATISHO NA. 8: Ajira Mpya na Mbadala kwa Mwaka 2014/2015.

ORODHA YA VIFUPISHO

ACBF	African Capacity Building Foundation
ACP	African Caribbean and Pacific
AfDB	African Development Bank
AGOA	African Growth and Opportunity Act
COMESA	Common Market for Eastern and Southern Africa
CPX	Command Post Exercise
DFID	Department for International Development
EAC	East African Community
EALA	East African Legislative Assembly
EPA	Economic Partnership Agreement
EU	European Union
FTX	Field Training Exercise
GIZ	Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit
ICF	Investment Climate Facility
JICA	Japan International Cooperation Agency
LVEMP	Lake Victoria Environmental Management Program
MKUZA II	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar,

	Awamu ya Pili
MKUKUTA	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
OSBPs	One Stop Border Posts
SADC	Southern Africa Development Community
SHIMIWI	Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali
TMEA	TradeMark East Africa
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
NACTE	Natonal Council for Technical Education
JAMAFEST	Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni Festival
IGAD	Intergovernmental Authority on Development
IMO	International Migration Organisation
ICF	Investment Climate Facility for Africa
UNHCR	United Nations High Commission for Refugees
APCPS	African Parliament Centre for Peace and Security
UTC	Union Trade Centre
ANAW	African Network for Animal Welfare
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini

DIRA NA DHIMA YA WIZARA

Dira

Kuwa na Jumuiya iliyoshamiri na inayowezesha Tanzania kunufaika kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Dhima

Kuhakikisha ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kujenga Jumuiya iliyoshamiri ni wenyе tija na unaolinda maslahi ya Taifa.

MISINGI YA UTENDAJI

- a. *Uadilifu*
- b. *Uzalendo*
- c. *Kujenga Uwezo Imara*
- d. *Uwajibikaji*
- e. *Huduma bora na sawia kwa wateja*
- f. *Utendaji wenyе tija*
- g. *Uwazi*
- h. *Huduma bila Upendeleo*
- i. *Ushirikiano*

**HOTUBA YA WAZIRI WA USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI, MHESHIMIWA
DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE (MB),
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA
KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

1.0 UTANGULIZI

- 1.** *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2015/2016.
- 2.** *Mheshimiwa Spika*, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala kwa ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo imekuwa ikiyatoa kwa Wizara yangu ili kuhakikisha ushiriki wa Tanzania katika Mtangamano wa Afrika Mashariki unakuwa na manufaa kwa Taifa na Watanzania kwa ujumla. Kamati hii ilipokea na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya

Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2015/2016 tarehe 06 Mei, 2015. Kamati ilitoa ushauri na hatimaye kuyapitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa kauli moja. Wizara imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati katika maandalizi ya Hotuba hii ya Bajeti.

3. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kuwa na imani na mimi na kunateua kuwa Waziri wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nitaendelea kufanya kazi kwa juhudini na maarifa na kuhakikisha fursa zilizopo katika mtangamano wa Afrika Mashariki zinatumika kikamilifu katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kuwaondolea wananchi umaskini.

4. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa namna ya pekee wananchi wa jimbo langu la Kyela kwa ushirikiano wao na kuendelea kuwa na imani nami katika kuleta maendeleo wilayani Kyela.

5. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Novemba, 2014 hadi Novemba, 2015, Tanzania ni mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuwa Mwenyekiti wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

6. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Bunge lako Tukufu lilipata simanzi kubwa kufuatia kifo cha aliyejkuwa Mbunge wa jimbo la Mbinga Magharibi Mhe. Kapt. John Damiano Komba. Nachukua fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, Wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi, familia ya marehemu na Watanzania kwa ujumla kwa kupotelewa na mwanasiasia mkongwe na mahiri. Mungu ailaze roho yake pema peponi.

7. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015 Nchi Mwanachama mwenzetu, Jamhuri ya Kenya ilikabiliwa na mashambulio mbalimbali ya kigaidi ikiwa ni pamoja na tukio lililotokea katika chuo Kikuu cha Garisa lililogharimu maisha ya watu wengi. Napenda kutoa pole kwa Mhe. Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya na wananchi wote wa Nchi hiyo kwa matukio hayo ya kinyama.

8. *Mheshimiwa Spika*, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Dkt. Abdulla J. Saadalla (Mb), Naibu Waziri; Bibi Joyce K.G. Mapunjo, Katibu Mkuu; Bw. Amantius

C. Msole, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo; na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipa na moyo wao wa kujituma katika utekelezaji wa majukumu na hivyo kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu.

9. *Mheshimiwa Spika*, uandaaji wa Hotuba hii umezingatia maudhui ya Hotuba ya Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa katika Bunge lako Tukufu ambayo imetoa mwelekeo na vipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2015/2016.

10. *Mheshimiwa Spika*, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu saba. Sehemu ya kwanza inatoa Utangulizi; sehemu ya pili ni Malengo na Mpango wa mwaka 2014/2015; na sehemu ya tatu ni Mapitio ya Utekelezaji wa Malengo na Mpango wa mwaka 2014/2015. Sehemu ya nne ni Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara; sehemu ya tano ni Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2015/2016; sehemu ya sita ni Shukrani; na sehemu ya saba ni Mawasilisho ya Maombi ya Fedha za Wizara katika mwaka 2015/2016.

2.0 MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

11. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara ilipanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i. Kuratibu maandalizi na kuongoza majadiliano katika mikutano ya Kisheria ya Wakuu wa Nchi Wanachama, Baraza la Mawaziri la Jumuiya, Mabaraza ya Mawaziri ya Kisekta ya Jumuiya, Vikundi Kazi na Wataalam;
- ii. Kuratibu na kufuutilia utekelezaji wa maamuzi ya Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya na Baraza la Mawaziri la Jumuiya;
- iii. Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Miaka Kumi wa Kuelekea Katika eneo la Sarafu Moja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- iv. Kuratibu uridhiwaji wa Itifaki mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizokwishesainiwa na Nchi Wanachama;
- v. Kuratibu Utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki;

- vi. Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (*EAC – EU Economic Partnership Agreement*);
- vii. Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano ya utatu wa COMESA-EAC-SADC;
- viii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Miradi na Programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na miradi ya uendelezaji wa miundombinu (barabara, reli, bandari, nishati, viwanja vya ndege) na miradi katika sekta ya kijamii na mazingira ya Jumuiya;
- ix. Kuratibu ujenzi wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja katika Mipaka ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na kuratibu uandaaji Sheria na Kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki za Uendeshaji wa Vituo vya kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani na Sheria ya Jumuiya ya Kudhibiti Uzito wa Magari;
- x. Kuratibu majadiliano ya uendelezaji wa Mradi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali/ Keza – Gitega – Musongati pamoja

na utafiti wa kuimarisha Sekta ya Reli utakaotoa mapendekezo ya kuanzisha njia mpya za reli;

- xii. Kuratibu Mapitio ya Mradi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuendana na mahitaji ya sasa kwa kuzingatia hatua zilizofikiwa na Nchi Wanachama katika kuendeleza Mtandao wa Mawasiliano;
- xiii. Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Mkakati wa Uwekezaji wa Miaka 5 (2013 – 2018) katika Sekta ya Hali ya Hewa na ukamilishaji wa Kanuni za Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Anga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- xiv. Kuandaa vigezo na viashiria vitakavyotumika kupima utekelezaji wa Mpango wa Uwazi katika Afya (*Open Health Initiative*);

- xv. Kuratibu Mpango wa kuziendeleza Taasisi tano zilizochaguliwa kuwa Taasisi za elimu zenyenye ubora uliobobeza za Jumuiya;
- xvi. Kuratibu tathmini ya utekelezaji wa Mradi wa Utunzaji wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria;
- xvii. Kuratibu utekelezaji wa mikakati ya uwianishaji wa Mifumo ya Elimu na Mitaala kwenye maeneo ya Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Mafunzo ya Ualimu, Mafunzo ya Makundi Maalumu, Mafunzo ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Mafunzo Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu ya Watu Wazima;
- xviii. Kuratibu uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha katika biashara baina ya Nchi Wanachama;
- xix. Kuratibu ushiriki katika Mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki (EALA) na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na mikutano kati ya Wizara na Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki;

- xx. Kukamilisha mapitio ya sheria za Tanzania ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- xxi. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano kuhusu Jamhuri za Sudan Kusini na Somalia kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- xxii. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano kuhusu Mpango Kazi na Modeli ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki;
- xxiii. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya maeneo ya kuwa na msimamo wa pamoja katika masuala ya Sera za Mambo ya Nje;
- xxiv. Kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuifanya Pasi ya kusafiria ya Afrika Mashariki kuwa ya Kimataifa;
- xxv. Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zilizopo kuititia Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara;

- xxvi. Kuratibu mapitio, utafiti, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mtangamano wa Afrika Mashariki;
- xxvii. Kuratibu utoaji wa huduma za masuala ya utumishi na utawala pamoja na kutekeleza masuala mtambuka (UKIMWI, Jinsia, na Utawala Bora);
- xxviii. Kuimarisha mifumo ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Mifumo ya Ununuzi pamoja na kuweka Mikakati ya Kusimamia Vihatarishi (*Risk Management Strategies*) vya utendaji wa Wizara; na
- xxix. Kuratibu uandaaji wa Mipango na Bajeti ya Wizara na taarifa mbalimbali za utendaji wa majukumu ya Wizara.

12. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 uliongozwa na vipaumbele vya Wizara vilivyobainishwa katika Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 ambao uliandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016); Mkakati wa Kukuza Uchumi na

Kupunguza Umaskini Tanzania Awamu ya Pili (MKUKUTA II), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar Awamu ya Pili (MKUZA II), Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango na Bajeti ya Serikali wa mwaka 2014/2015 na Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2013/2014 – 2017/2018.

13. *Mheshimiwa Spika*, aidha, mpango huo ulizingatia Mkakati wa Nne wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2011/2012-2015/2016; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Maagizo ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya. Mapendekezo ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016 yameandaliwa kwa kuzingatia Miongozo hii ya Kitaifa na Kikanda.

14. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliidhinishiwa Shilingi 23,057,859,000 ambapo Shilingi 21, 524,605,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na Shilingi 1,533,254,000 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2015, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 18,591,993,810 kutoka Wizara ya Fedha; Shilingi 1,406,070,660 zikiwa ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 17,185,923,150 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Katika kiasi cha fedha kilichopokelewa cha Matumizi Mengineyo, Shilingi 13,678,183,750 zilikuwa kwa ajili ya mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Shilingi 3,507,739,400 zilitumika kutekeleza majukumu mengine ya Wizara.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO NA MPANGO WA MWAKA 2014/2015

3.1 SERA NA MIKAKATI

- a. Sera ya Takwimu za Hali ya Hewa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Meteorological Data Policy*)**

15. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua ya utekelezaji wa Sera ya Takwimu za Sekta ya Hali ya Hewa (*EAC Meteorological Data Policy*) mwaka 2014/2015, viliandaliwa vipaumbele vinne vya utekelezaji wa Sera hiyo katika ngazi ya Nchi Wanachama. Maeneo ya vipaumbele ni pamoja na upatikanaji, usambazaji, uchambuzi na ubadilishanaji wa takwimu za hali ya hewa. Aidha, ili kuwezesha utekelezaji wa sera hii Nchi Wanachama zinatakiwa kuandaa/kufanya mapitio katika sera zao za kitaifa zinazohusu masuala ya hali ya hewa.

b. Sera ya Mifugo ya Afrika Mashariki

16. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano ya uandaaji wa Sera ya Mifugo ya Jumuiya Afrika Mashariki. Lengo la Sera hiyo ni kuweka mazingira bora ya ufugaji; kuendeleza taasisi za mafunzo ya ufugaji wa aina mbalimbali na kuanzisha taasisi ya fedha ya Jumuiya kwa ajili ya kuhudumia wafugaji na hivyo kuongeza tija katika sekta ya mifugo. Kimsingi será hii imeidhinishwa na Jumuiya ambapo kwa sasa Nchi Wanachama zinaandaa mkakati wa utekelezaji wake.

c. Sera ya Usalama wa Chakula na Lishe ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

17. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Nchi Wanachama zilikamilisha majadiliano ya uandaaji wa rasimu ya Sera ya Usalama wa Chakula na Lishe ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayolenga kuziwezesha Nchi Wanachama kuwa na mkakati endelevu wa uhakika wa chakula na lishe bora katika kipindi chote cha mwaka. Sera hii imejikita katika kuimarishe uzalishaji na usindikaji, uhifadhi wa chakula, kuongeza ajira zitokanazo na shughuli za kilimo, kuhuishwa biashara ya chakula ndani na nje ya Jumuiya, kuboresha upatikanaji wa chakula katika maeneo

yenye uzalishaji mdogo na kuhimiza ubora na viwango vya bidhaa za vyakula. Kimsingi será hii imeidhinishwa na Jumuiya na Tanzania inaendelea na mashauriano ya ndani ili kuhakikisha utekelezaji wa sera hii unakuwa na manufaa Kitaifa.

3.2 UTEKELEZAJI WA HATUA ZA MTANGAMANO

18. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa hatua za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ifuatavyo:

3.2.1 Umoja wa Forodha

a. Utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha

19. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha. Mfumo huu unawezesha waagizaji wa bidhaa zinazotoka nje ya Afrika Mashariki kwenda nchi yoyote ile mwanachama wa Jumuiya kukamilisha taratibu zote za kiforodha mahali bidhaa zilipoingilia. Aidha, kupitia mfumo huu malipo yatafanyika kwenye nchi shehena inapokwenda na

mamlaka ya forodha ya nchi hiyo mwanachama itawasilisha taarifa kwa mamlaka ya forodha mzigo ulipoingilia ili kuruhusu shehena kuondoshwa na kusafirishwa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia shehena (*electronic cargo tracking system*).

20. *Mheshimiwa Spika*, mfumo huu unaondoa urasimu uliokuwepo kwa miaka mingi wa kukamilisha taratibu za kiforodha kwenye kila mpaka na kusababisha ucheleweshaji mkubwa wa bidhaa na ongezeko kubwa la gharama za uchukuzi na ufanyaji biashara kwa ujumla. Utekelezaji wa mfumo huu kwa majaribio kwenye ukanda wa uchukuzi wa Kaskazini ambao unahusisha nchi za Kenya, Uganda na Rwanda, ulianza Januari, 2014, wakati utekelezaji wa majaribio kwa ukanda wa uchukuzi wa kati unaozihusisha nchi za Tanzania, Uganda Rwanda na Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ulianza mwezi Juni, 2014.

21. *Mheshimiwa Spika*, matokeo ya majaribio haya kwa kanda zote mbili umeonesha kuwa gharama za kufanya biashara (*Costs of Doing Business*) zimepungua kwa takribani asilimia hamsini ikiwemo muda wa kusafirisha bidhaa kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda Bujumbura kupitia mpaka Kabanga/Kobero na kwenda Kigali kupitia mpaka wa Rusumo

umepungua kutoka siku 10 mpaka siku 4 hadi 6 kwa sehemu zote mbili. Aidha, muda wa kusafirisha bidhaa toka bandari ya Mombasa mpaka Kampala, Uganda na mpaka Kigali, Rwanda umepungua toka siku 18 hadi siku 4 na kutoka siku 21 hadi siku 6 sawia. **Kiambatisho Na. 1** kinaonesha bidhaa ambazo zinatumia mfumo huu katika kipindi hiki cha majaribio.

22. *Mheshimiwa Spika*, kazi kubwa ya maandalizi imefanyika na inaendelea kufanyika kuwezesha mfumo huu kufanya kazi vizuri zaidi kama ifuatavyo:

- (i) uandaaji na utekelezaji wa taratibu za pamoja za kiforodha;
- (ii) urahisishaji wa uwekaji wa Dhamana (*Bond*) kwa kuwa na Dhamana moja ya Jumuiya (*Regional Bond*) kwa mizigo inayokwenda Nchi Wanachama yenye misamaha ya Kodi;
- (iii) uoanishaji wa mifumo ya TEHAMA inayotumika na Nchi Wanachama katika kuondosha na kupokea shehena;
- (iv) utoaji mafunzo kwa wadau mbalimbali wanaotumia mifumo hiyo ya TEHAMA;

- (v) kuandaa ofisi za pamoja za forodha kwenye bandari zetu kuu za Dar es Salaam na Mombasa ambapo maofisa wa forodha toka nchi husika wanachama wanafanya kazi kwa kushirikiana. Kwa mfano, Tanzania tayari imepeleka maofisa wake wa forodha Nairobi na bandari ya Mombasa. Aidha, Burundi na Rwanda zimekwishaleta maofisa wao wa forodha bandari ya Dar es Salaam, wakati Kenya na Uganda zinakamilisha taratibu husika za kuleta maofisa wao. Kukamilika kwa utaratibu huu kutaongeza kasi ya utoaji wa shehena zinazokwenda katika nchi hizo;
- (vi) Kuundwa kwa Kamati ya Kitaifa ya kusimamia utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha chini ya Wizara ya Fedha ambayo pamoja na mambo mengine itakuwa na wajibu wa kupendekiza namna ya kurahisisha taratibu za upakuaji na usafirishaji shehena bandarini na katika vituo vingine vya forodha;
- (vii) Uanzishaji wa mfumo maalum wa kielekitroniki wa ufuatiliaji wa mizigo

(electronic cargo tracking system) kwa lengo la kuhakikisha mizigo inayokwenda nje ya nchi (*transit cargo*) inafika katika nchi iliyokusudiwa. Pamoja na faida za mfumo huu nilizolezea awali, utekelezaji wake kikamilifu utaongeza mapato ya Serikali kupitia mfumo wa kikanda wa kuzuia magendo na kupunguza uwezekano wa bidhaa zinazopitia nchini kuishia katika soko la ndani bila ya kulipiwa kodi stahiki;

(viii) Bunge la Afrika Mashariki limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Umoja wa Forodha wa mwaka 2015 (*The East African Community Customs Management (Amendment) Bill, 2015*) ili kuwezesha utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha.

b. Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha

23. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Kamati ya Kitaifa ya Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha imeendelea na kazi yake ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2015 Vikwazo Visivyo vya Kiforodha 101 vimeripotiwa.


Kati ya hivyo, vikwazo 83 vilipatiwa ufumbuzi na hatua ya kuvipatia ufumbuzi vikwazo 18 bado zinaendelea. Kwa upande wa Tanzania vikwazo ambavyo vimekuwa vikijitokeza ni pamoja na vizuizi vya Polisi katika njia ya Kati (Dar es Salaam hadi Rusumo Mpakani), kupimwa kwa malori yasiyo na mizigo na yenye makontena matupu.

24. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi imepiga hatua kubwa katika kushughulikia vikwazo hivyo. Moja ya hatua tulizozichukuwa kama Serikali ni ujenzi wa vituo vya pamoja vya kufanya ukaguzi barabarani (*one stop inspection centres*). Vituo hivyo kwa upande wa ukanda wa kati wa uchukuzi ni vitatu: Vigwaza (mkoani Pwani), Manyoni (mkoani Singida) na Nyakanazi (mkoani Kagera). Kituo cha Vigwaza ambacho kimewekewa mitambo ya kisasa ya upimaji uzito wa magari huku yakitembea, kimeanza kutumika kwa majaribio na hivyo kupunguza msongamano mkubwa wa malori uliokuwepo awali kwenye mizani ya Kibaha ambayo sasa haipo. Ujenzi wa vituo vingine viwili upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na vyote vitawekewa mizani ya kisasa ya kupima malori yakiwa yanatembea, hivyo kuondokana kabisa na tatizo la misururu mirefu ya kupima magari kwenye mizani.


c. Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa kati ya Tanzania na Nchi Wanachama za Jumuiya

25. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, biashara baina ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliendelea kukuwa na kufikia Dola za Marekani milioni 5,805.6 mwaka 2013 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 3,722.88 za mwaka 2010. Aidha, biashara baina ya Tanzania na Nchi Wanachama imeendelea kuimarika na kuongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 690.2 mwaka 2010 na kufikia Dola za Marekani milioni 1,310.9 mwaka 2014. Pamoja na Kenya kuendelea kuongoza katika soko la Jumuiya (41% mwaka 2010 na 31% mwaka 2013), nafasi ya Tanzania imeendelea kupanda kutoka asilimia 18% mwaka 2010 hadi 26% mwaka 2013 na kushika nafasi ya pili, huku dalili za kufanya vema zaidi zikijitokeza bayana ikiwa juhudzi zinazoendelea za kudhibiti ulanguzi wa mazao na bidhaa mipakani na kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha zitafaulu. **Matufe Na. 1 na Na. 2** hapa chini yanaonesha mgawanyo wa soko baina ya Nchi Wanachama mwaka 2010 na mwaka 2013. Aidha, **Kiambatisho Na. 2** kinabainsisha mwenendo wa Biashara ya jumla (Mauzo na Manunuzi), baina ya Nchi Wanachama.

Tufe Na. 1: Mgao wa Soko katika mwaka 2010.



Tufe Na. 2: Mgao wa Soko katika mwaka 2013.



26. *Mheshimiwa Spika*, bidhaa zilizouzwa zaidi ni mbegu za mahindi, katani, mbogamboga, mahindi, mashudu ya mifugo, neti za mbu, saruji, na magunia. Hii inaashiria kuendelea kuimarika kwa biashara ya mazao ya kilimo na uzalishaji viwandani kutokana na wafanyabiashara wa Tanzania kuendelea kuchangamkia fursa zitokanazo na Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Aidha, bidhaa zilizoingizwa kwa wingi kutoka Nchi Wanachama ni pamoja na kemikali kwa ajili ya viwanda vya nguo, vipodozi na sabuni, dawa za binadamu na mifugo, vipuri vya magari, vifuniko vya kufungia chupa za vinywaji, sabuni, vifaa vya kufanya usafi, vifungashio, mabanda maalum ya kilimo cha mbogamboga na maua (*green houses*) na vyumba vya baridi kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa mbalimbali (*cold rooms*).

d. Uwekezaji

27. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki umeendelea kuchangia katika jitihada za Serikali za kuvutia na kukuza uwekezaji hapa nchini. Katika kipindi hiki jumla ya miradi 40 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 101.14 iliwekezwa hapa nchini kutoka Nchi Wanachama. Nafasi za ajira zilizozalishwa kutokana na uwekezaji huo ni 1,233. **Kiambatisho Na. 3** kinaonesha miradi iliyowekezwa hapa nchini kutoka Nchi Wanachama, thamani na ajira zilizozalishwa katika mwaka 2014. Aidha, makampuni ya Tanzania kama vile Benki ya CRDB (imefungua matawi nchini Burundi), Chemi and Cotex (Rwanda na Kenya), Mt.Meru Oil (Rwanda), Mikoani Traders (Rwanda) na SS Bakhresa (imewekeza katika nchi zote wanachama wa Jumuiya) yameendelea kutumia fursa ya uwekezaji katika Nchi Wanachama.

28. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua ya kuwawezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati kuwekeza na kufanya biashara katika Nchi Wanachama, kila mwaka hufanyika maonesho ya biashara ya Jumuiya ya Juakali/Nguvukazi. Maonesho hayo ambayo hufanyika kwa mzunguko baina ya Nchi Wanachama, huwawezesha Wajasiriamali kutoka Tanzania kupata fursa ya

kutangaza na kuuza bidhaa zao za batiki, vikoi, bidhaa za kilimo zilizosindikwa, sanaa za mikono, bidhaa za ngozi, uhunzi na madawa ya tiba asili katika Nchi Wanachama. Aidha, huwawezesha pia kujifunza, kujenga mitandao ya biashara na kujijengea uwezo wa kiushindani kwa kuimarisha zaidi ubora wa bidhaa zao. Katika mwaka wa fedha 2014 maonesho hayo yalifanyika Nchini Rwanda ambapo jumla ya wafanyabiashara ndogondogo na wa kati 120 kutoka Tanzania walishiriki. Maonesho ya 16 yatafanyika Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa mwezi Novemba, 2015. Kaulimbiu ya maonesho hayo itakuwa “*Nunua Bidhaa za Wajasiri amali wa Afrika Mashariki Kuijenga Afrika Mashariki*”.

3.2.2 Soko la Pamoja la Afrika Mashariki

29. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015, Wizara ilikamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja na kwa sasa tupo katika hatua za mwisho za kuidhinisha Mkakati huo ili kuwezesha utekelezaji wake kuanza.

30. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua ya kupunguza biashara za mipakani zisizotumia njia rasmi, Wizara imeendelea kuhimiza, kutoa elimu na kushawishi wafanyabiashara wengi hususan

wadogo na wa kati kuzitumia fursa za Soko la Pamoja kwa mfano upelekaji wa bidhaa zinazozalishwa nchini kwenye masoko ya Nchi Wanachama bila kulipia ushuru. Katika mwaka 2014/2015 vyeti 5,451 vilivyorahisishwa au kufafanuliwa vizuri vya kutambua uasili wa biadhaa vilitolewa kwa wafanyabiashara wenye nia ya kuuza bidhaa kwenye masoko ya Nchi Wanachama ikilinganishwa na vyeti 3,895 vilivyotolewa mwaka 2013/2014. Ni azma ya Wizara kuisogeza huduma hii karibu na wadau wote nchini wenye ari ya biashara.

31. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta imeendelea kubainisha sheria za ndani zinazotakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuwzesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja na hivyo kuwawezesha Watanzania na wananchi wa Afrika Mashariki kunufaika na fursa zitokanazo na Soko hilo. Wizara imeendelea kufuatilia na kuzihimiza Wizara za kisekta kutoa uzito stahiki katika zoezi la kurekebisha sheria husika. Pamoja na ucheleweshaji huo tumeweza kutunga Sheria ya Kuratibu Ajira ya Wageni ya mwaka 2015 ambayo imezingatia matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja. Sheria zilizochambuliwa na kubainishwa kuwa zinatakiwa kufanyiwa marekebisho ni pamoja na: Sheria zinazohusu Sekta ya Elimu Tanzania ikiwa ni pamoja na Sheria ya Vyuo Vikuu Sura ya 346

na Kanuni zake za mwaka 2013, Sheria ya Baraza la Elimu ya Ufundu Tanzania (NACTE) Sura ya 129 na Kanuni zake za mwaka 2001, Sheria ya Mamlaka ya Elimu ya Ufundu Stadi (VETA) ya mwaka 1994 na Sheria ya Usajili wa Wasanifu na Wakadiriaji wa Majengo Na. 4 ya mwaka 2010.

3.2.3 Umoja wa Fedha

32. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Nchi Wanachama ziliridhia Itifaki ya Umoja wa Fedha ambapo Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kufanya hivyo. Uridhiwaji wa Itifaki hii umewezesha kuanza kwa utekelezaji wa Mpango Kazi wa miaka kumi wa kuelekea katika eneo la Sarafu Moja ifikapo mwaka 2024. Utekelezaji wa Mpango Kazi huo unahusisha kuanzisha Taasisi zifuatazo: Taasisi ya Fedha; Taasisi ya Takwimu; Taasisi za Huduma za Fedha na Taasisi ya Usimamizi na Ufutiliaji wa Utekelezaji wa Umoja wa Fedha. Nchi Wanachama zimeunda Kikosi Kazi cha kuandaa miswada ya sheria ya kuanzisha taasisi hizi. Kwa upande wa Tanzania, Taasisi zinazoshiriki katika Kikosi Kazi hiki ni Wizara ya Fedha, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Benki Kuu ya Tanzania, Taasisi ya Takwimu na Taasisi ya Usimamizi wa Hifadhi za Jamii.

3.2.4 Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki

33. *Mheshimiwa Spika*, Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki ni hatua ya nne na ya mwisho katika mtangamano wa Afrika Mashariki. Nchi Wanachama wa Jumuiya zinaendelea na majadiliano ya Muundo na Modeli ya litakalokwa na Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Hii ni kufuatia maagizo ya Wakuu wa Nchi Wanachama katika Mkutano wao wa 12 wa Dharura uliofanyika mwezi Aprili, 2014 pamoja na mambo mengine walielekeza Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzisha mchakato wa uandaaji wa rasimu ya Katiba ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki na Mpango Kazi wa masuala ya kutekelezwa ili kuweza kuandaa Katiba ya Shirikisho husika. Katika kutekeleza maamuzi ya Wakuu wa Nchi, Nchi Wanachama zimekuwa na majadiliano ya aina ya muundo wa Shirikisho la Kisiasa ikiwa ni hatua ya msingi ya kuelekea katika kuandaa Katiba ya Shirikisho.

3.3 USHIRIKIANO NA KANDA NYINGINE ZA KIUCHUMI

3.3.1 Ushirikiano wa Utatu wa COMESA- EAC- SADC

34. *Mheshimiwa Spika*, ushirikiano wa Utatu wa COMESA-EAC-SADC umejengwa katika mihimili mitatu ya uchumi ambayo ni Mtangamano wa Masoko; Maendeleo ya Miundombinu; na Maendeleo ya Viwanda. Katika Muhimili wa mtangamano wa masoko, Nchi Wanachama zimekubaliana kuanzisha Eneo Huru la Biashara. Aidha, nchi wanachama zimekubaliana kufanya majadiliano kuhusu Uhuru wa Wafanyabiashara Kusafiri Katika Eneo Huru la Biashara la Utatu. Hatua iliyofikiwa katika majadiliano kwa mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:

a) Eneo Huru la Biashara la Utatu

35. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015, jumla ya nchi 20 zilikuwa zimekamilisha maandalizi ya mapendekezo ya kupunguziana ushuru (*tariff offers*) na kuanza majadiliano. Majadiliano ya kupunguziana ushuru baina ya

Jumuiya ya Afrika Mashariki na Misri yalifanyika na pande zote mbili kubadilishana mapendekezo ya kupunguziana ushuru ambapo Misri iko tayari kufungua masoko yake kwa asilimia mia moja kwa nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mapendekezo ya Tanzania ni kupunguza hatua kwa hatua ambapo kwa kuanzia soko litafunguliwa kwa asilimia 96.89 na asilimia zilizosalia (3.11%) zitapunguzwa katika kipindi cha miaka mitano.

36. *Mheshimiwa Spika*, Nchi Wanachama zimekamilisha majadiliano ya rasimu ya Mkataba wa kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC na mkataba huo unatarajiwa kusainiwa na Wakuu wa Nchi na Serikali mwezi Juni, 2015. Aidha, majadiliano yataendelea katika baadhi ya viambatisho vya Mkataba ambavyo havijakamilika. Viambatisho hivyo ni pamoja na vigezo vya utambuzi wa Uasilia wa Bidhaa; na Kanuni za Usuluhihi wa Migogoro ya Kibashara.

37. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania ambayo ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC iliwasilisha maombi ya kuwa mwenyeji wa Sekretarieti ya Utatu wa COMESA-EAC-SADC ambapo kama itakubalika Makao Makuu yake yanatarajiwa kuwa Jiji Arusha, Tanzania.

**b) Uhuru wa Wafanyabiashara Kusafiri
Katika Eneo Huru la Biashara la
Utatu**

38. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kuratibu majadiliano ya Rasimu ya makubaliano ya uhuru wa wafanyabiashara kusafiri katika Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 Kamati ya majadiliano ilikamilisha mapitio ya Kanuni na taratibu za uhamiaji zinazotumika katika Nchi Wanachama. Lengo la mapitio haya ni kuandaa Mkataba utakaotoa uhuru kwa wafanyabiashara kusafiri katika Eneo la Utatu ambapo majadiliano ya Ibara 22 kati ya 25 za rasimu ya Mkataba yamekamilika.

39. *Mheshimiwa Spika*, majadiliano yanaendelea katika Ibara ya 5 inayohusu Kanuni zitakazoongoza utekelezaji wa Mkataba (*Guiding principles*); Ibara ya 9(1) inayohusu taratibu za maombi, utoaji Visa na muda wa wafanyabiashara kukaa katika Nchi Wanachama pamoja na utaratibu wa kupata Visa mpya baada ya ukomo wa Visa ya awali; na Ibara ya 16 inayohusu mfumo wa utatuzi wa migogoro (*Dispute Settlement Mechanism*).

c) Uendelezaji wa Viwanda Katika Eneo la Utatu wa EAC-COMESA-SADC

40. *Mheshimiwa Spika*, Nchi Wanachama zimekubaliana kushirikiana katika maeneo ya Uratibu na Uhamasishaji wa pamoja wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda; Uhamasishaji wa kimkakati wa uongezaji wa thamani za bidhaa baina ya Nchi Wanachama; Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na vya Kati na kujenga uwezo na Utaalam katika kuendeleza Viwanda.

41. *Mheshimiwa Spika*, masuala mengine yaliyokubalika ni Eneo la Viwango, Kanuni za Kitaalam na Uhakiki wa Ubora wa Bidhaa; Utafiti na Maendeleo kwa ajili ya kukuza teknolojia, uvumbuzi na uuzaji; Kulinda Hati Miliki na Kuendeleza Mifumo ya Utaalam wa Asili na Ushirikiano wa Kimataifa katika kuendeleza Viwanda. Nchi Wanachama zimekubaliana pia kushirikiana katika Uendelezaji wa Miundombinu ya Viwanda; Takwimu za Viwanda na Ubadilishanaji wa Taarifa mbalimbali za masuala yanayohusu maendeleo ya Viwanda; na Utafutaji wa Rasilimali Fedha kwa ajili ya kuendeleza Viwanda vya Kikanda.

3.3.2 Ubia wa Kiuchumi Kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (EAC-EU Economic Partnership Agreement – EPA)

42. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015 majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya yalikamilika na Mkataba uliwekwa saini za awali (*initialing*) mwezi Oktoba 2014.

43. *Mheshimiwa Spika*, Mkataba wa EPA umejumuisha sura ya ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo yenye miradi ya maendeleo pamoja na kuwepo kwa Mfuko wa EPA utakaowezesha kukabiliana na gharama zitokanazo na utekelezaji wa Mkataba wa EPA. Mfuko huu pia utawezesha Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kukabiliana na changamoto za uzalishaji na usambazaji zinazofanya nchi hizo kushindwa kunufaika na fursa mbalimbali za masoko ya Jumuiya ya Ulaya na duniani kwa ujumla.

44. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia makubaliano kuwekewa saini za awali, hatua inayofuata ni kuuweka mkataba katika lugha ya kisheria na hatimaye kutafsiriwa katika lugha 21 zinazotumiwa na nchi za pande mbili za mkataba ikiwa ni pamoja na lugha ya Kiswahili

inayotumika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kabla ya kusainiwa.

45. *Mheshimiwa Spika*, malengo ya ubia huu ni kuimarisha ushirikiano wa kikanda, kuleta maendeleo endelevu, kupunguza umaskini kwa kuziwezesha nchi za *Africa, Caribbean na Pacific (ACP)* kukabiliana na changamoto za uzalishaji na kuweka muda wa kuondoa vikwazo vya biashara ili kuzilingiza Nchi hizo katika uchumi wa dunia.

3.3.3 Mkataba wa Ubia wa Biashara na Uwekezaji Baini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani.

46. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani zilisaini makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya Uwezeshaji wa Kibiashara (*Trade Facilitation*), Viwango vya Afya ya Mimea na Wanyama (*Sanitary and Phyto-sanitary*) na Uondoaji wa Vikwazo vya Kiufundi katika Biashara (*Technical Barriers to Trade*). Ushirikiano huu unalenga pamoja na mambo mengine kuzijengea uwezo Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika maeneo ya rasilimali watu na fedha ili kuwa na biashara zenye tija baina ya pande zote mbili.

47. *Mheshimiwa Spika*, aidha, Jumuiya yetu na Marekani tuliweza kujadiliana kuhusu fursa na changamoto mbalimbali zinazolikabili Soko la A GOA na kukubaliana kuwa uandaliwe mkakati wa A GOA wa Afrika Mashariki. Kwa kuwa mkataba wa A GOA utafikia kikomo mwezi Septemba, 2015, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeiomba Marekani kuharakisha mchakato wa kuongeza kipindi kingine cha A GOA kwa muda mrefu zaidi ili kuvutia wawekezaji wengi toka Marekani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

3.4 USHIRIKIANO KATIKA SEKTA ZA UZALISHAJI

48. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliendelea na majadiliano na utekelezaji wa masuala mbalimbali yanayohusu ushirikiano katika sekta za uzalishaji kama ifuatavyo:

- a. Uendelezaji wa Viwanda Katika Jumuiya**

49. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua ya utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Viwanda wa Afrika Mashariki, Jumuiya imeandaa taarifa ya

mzunguko wa thamani katika bidhaa (*Value Chain*) za sekta sita za kipaumbele zilizoainishwa katika mkakati husika. Sekta hizo zinahusu usindikaji wa mazao, bidhaa za petroli na gesi na chuma na madini; uendelezaji wa nishati Jadidifu; uzalishaji wa mbolea na dawa za kilimo; na uzalishaji wa dawa za binadamu.

50. *Mheshimiwa Spika*, Jumuiya ya Afrika Mashariki imekamilisha utafiti wa namna ya kuongeza thamani katika bidhaa za chuma ambao unatoa mapendekezo ya namna ya kuongeza tija katika sekta ya chuma na bidhaa zake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

51. *Mheshimiwa Spika*, vilevile utafiti huo umebainisha kuwepo kwa kiasi cha tani bilioni 2.8 za madini ya chuma katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambacho kinaweza kuchimbwa kwa muda wa miaka 560. Aidha, kiasi hicho kinaweza kuongezeka na kufikia zaidi ya tani bilioni 10 endapo maeneo ya utafiti yatapanuliwa. Utafiti huo umeonesha pia kuwepo kwa kiasi cha gesi asilia mita za ujazo (*cubic metre feet*) trilioni 50.5 na makaa ya mawe tani bilioni 2.4 katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

52. *Mheshimiwa Spika*, Utafiti huo pamoja na mambo mengine unapendekeza kuanzisha makampuni makubwa ya kitaifa na kikanda ya

uchimbaji na uchakataji wa chuma; Nchi Wanachama kujenga miundombinu muhimu kwenye maeneo yenyе rasilimali za chuma; kuandaa sera ya kuongeza ushiriki wa makampuni ya ndani katika ujenzi wa miundombinu ya kijamii; kuweka sera ya kuwezesha makampuni yaliyopo katika Nchi Wanachama kununua malighafi ndani ya Jumuiya; na kuandaa tovuti maalum itakayokuwa na taarifa zote muhimu kutoka Nchi Wanachama ili kuvutia uwekezaji kwenye sekta hizo. Mapendekezo haya yamewasilishwa katika Nchi Wanachama kwa ajili ya kuyatolea maoni.

53. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2014/15, Wizara imeratibu na kushiriki katika utafiti wa mzunguko wa thamani katika sekta ya kilimo (*Agro-Industry Value Chain*). Utafiti huo umehusisha ngozi na bidhaa za ngozi, pamba, sukari, maziwa, nyama, mahindi na matunda. Utafiti huo ambao unaendelea utasaidia kubainisha bidhaa ambazo Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zitatakiwa kuziandalia Mpango Kazi kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na uongezaji wa thamani wa bidhaa hizo ndani ya Jumuiya.

54. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Jumuiya iliendelea na maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Kuendeleza Viwanda ikiwa ni utekelezaji wa Sera na Mkakati wa kuendeleza viwanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sheria hii pamoja na mambo mengine itaiwezesha Jumuiya kuchukua hatua za haraka na madhubuti katika kuongeza kasi ya uendelezaji wa viwanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

55. *Mheshimiwa Spika*, ili kuwaleta pamoja wazalishaji wa viwandani na sekta za teknolojia pamoja na kufungua fursa za biashara, kutafanyika Kongamano la kwanza la Uzalishaji Viwandani na Biashara ya Teknolojia mwezi Septemba 2015, Kampala, Uganda. Katika Kongamano hilo makampuni ya ndani kutoka Nchi Wanachama yatapata fursa ya kubadilishana uzoefu na makampuni makubwa ya nje ya Jumuiya na hivyo kuhamasisha uzalishaji wenye tija na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika sekta ya viwanda.

b. Itifaki ya Utalii na Wanyamapor

56. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki, Nchi Wanachama zilikamilisha majadiliano ya Itifaki ya Utalii na Wanyamapor ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la Itifaki hii ni kuimarisha ushirikiano baina ya Nchi Wanachama katika

kuendeleza sekta ya utalii na wanyamapori na kuhakikisha kunakuwepo na uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

c. Mradi wa Jumuiya wa Kukabiliana na Athari za Sumukuvu (*Aflatoxin*)

57. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015 Jumuiya iliendelea na utekelezaji wa mradi wa kikanda wa kukabiliana na athari za sumukuvu. Mradi huu unalenga kuelimisha jamii juu ya tatizo la sumukuvu inayopatikana katika mazao ya vyakula, kuimarisha udhibiti wa sumukuvu kupitia hatua mbalimbali za biashara ya mazao na kudhibiti sumukuvu katika mazao yakiwa shambani. Mafanikio ya utekelezaji wa Mradi huu utafungua milango ya masoko ya Ulaya na Marekani kwa bidhaa za Kilimo kutoka Nchi za Afrika ya Mashariki ambazo kwa sasa hazipewi nafasi kutokana na changamoto mbalimbali za ubora wa mazao likiwemo tatizo la Sumukuvu.

3.5 UENDELEZAJI WA MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI

58. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa programu na miradi ya kikanda ya

uendelezaji wa Miundombinu ya Kiuchumi kama ifuatavyo:

**a) Uendelezaji wa Barabara
Zinazounganisha Nchi Wanachama**

59. *Mheshimiwa Spika*, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa kuendeleza Mtandao wa Barabara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hiki, mtandao wa barabara wa Afrika Mashariki umefanyiwa marekebisho na kuwa na kanda kumi (10) ikilinganishwa na tano za awali. Marekebisho hayo yamefanyika kwa lengo la kurahisisha ufuatiliaji wa uendelezaji wa miundombinu ya barabara zinazounganisha Nchi Wanachama. Kanda hizo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 4** Hatua zilizofikiwa katika uendelezaji wa mtandao wa barabara kwenye kanda hizo katika mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:

i. Barabara ya Malindi – Mombasa - Lungalunga/Tanga – Bagamoyo

60. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Barabara ya Malindi – Mombasa - Lungalunga/Tanga – Bagamoyo uliendelea katika kipindi hiki ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulikamilika. Aidha,

Mshauri Mwelekezi ameagizwa na Kamati ya Usimamizi wa Utekelezaji wa mradi kufanya utafiti zaidi wa miamba (*Geotechnical Survey*) hususan katika daraja la mto Wami na Pangani ili kuwa na uhakika zaidi wa hali ya miamba katika maeneo yatakayojengwa madaraja hayo. Aidha, kufuatia upungufu uliobainika katika taarifa ya Mshauri Mwelekezi, Kamati iliunda Timu ya Wataalam kutoka Nchi Wanachama kwa ajili ya kuhakiki na kutoa ushauri. Timu ya Wataalam imeshauri kuwa daraja la mto wami liwe na urefu wa mita 540 badala ya kilometra 1.34. Kwa kuzingatia ushauri huo, Kamati imemwagiza Mshauri Mwelekezi kurekebisha michoro ili daraja lijengwe kwa kuzingatia ushauri wa Timu ya Wataalam.

**ii. Mradi wa Barabara ya Arusha –
Holili/Taveta – Voi**

61. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu uendelezaji wa mtandao wa barabara unaozunganisha nchi za Tanzania na Kenya kupitia mpaka wa Holili/Taveta. Aidha, barabara hii inaunganisha Kanda za Kaskazini na Kati kutoka Tanzania hadi Kenya kupitia mpaka wa Holili/Taveta. Katika mwaka 2014/2015 majadiliano ya Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Sakina – Tengeru *Dual Carriageway* (14.1 km) na mchepuko wa Arusha (42.4 km) yamekamilika na Mkataba wa ujenzi ulisainiwa mwezi Februari,

2015. Aidha, kwa kipande cha Tengeru – Holili na Barabara ya kuelekea uwanja wa ndege wa Kilimanjaro (108 km); hatua ya kutafuta fedha za ujenzi zinaendelea.

iii. Barabara ya Arusha – Namanga

62. *Mheshimiwa Spika*, barabara ya Arusha – Namanga ilikamilika na kufunguliwa mwaka 2012. Katika hatua ya kuhakikisha barabara hii inadumu kwa muda mrefu, imekubalika kuwa barabara zilizopo pembedi mwa barabara hii zitengenezwe kwa kiwango cha lami. Aidha, maboresho ya upungufu uliobainishwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara hii ikiwemo kipande cha km 32 hadi km 41.5 kutoka Arusha kuelekea Namanga na miundombinu ya ziada ya kupitisha maji yamekamilika.

b) Vituo Vya Utoaji wa Huduma kwa Pamoja Mipakani

63. *Mheshimiwa Spika* katika kipindi hiki, Wizara iliratibu ukamilishaji pamoja na kusainiwa kwa Mwongozo na Taratibu za Uendeshaji wa Vituo vya Utoaji wa Huduma kwa Pamoja Mipakani katika mipaka kati ya Tanzania na Kenya (Namanga, Holili, Horohoro na Sirari) na Rwanda (Rusumo). Aidha, majadiliano ya ukamilishaji wa Kanuni za Utekelezaji wa Sheria

ya Jumuiya ya Kusimamia Uendeshaji wa Vituo vyta Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani yanatarajiwa kukamilika mwaka 2015/2016.

64. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Vituo vyta Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na 5**. Aidha, ufunguzi wa vituo vilivyokamilika unatarajiwa kufanyika kabla ya mwisho wa mwaka 2015.

65. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa daraja la Kimataifa la Rusumo ambalo ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa Kituo cha Utoaji Huduma kwa Pamoja cha Rusumo umekamilika. Daraja hilo lina uwezo mkubwa kuliko daraja la awali kwani lina uwezo wa kupitisha magari manne kwa wakati mmoja yenye uzito wa tani 56 kila moja.

c) Uwianishaji wa Uzito wa Magari Katika Barabara

66. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliratibu maandalizi ya Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Jumuiya ya Udhibiti wa Uzito wa Magari iliyopitishwa na Bunge la Afrika Mashariki mwaka 2013. Kanuni hizi zinatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka 2015/2016.

d) Uendelezaji wa Mtandao wa Reli Katika Jumuiya

67. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015 Wizara iliratibu upatikanaji wa maoni kuhusu utafiti wa kuboresha miundombinu ya reli katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unaofanywa na Mshauri Mwelekezi kutoka Canada (*CPCS Transcom*). Utafiti huo ulioanza mwezi Februari, 2014 na ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2015 utatoa ushauri wa namna ya kutekeleza mapendekezo yaliyoainishwa katika Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Reli katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, utafiti huo utatoa mapendekezo ya mfumo wa ushirikiano katika sekta ya reli kwa Nchi Wanachama na mwongozo wa namna ya kutekeleza miradi ya kipaumbele inayouzika kwa wafadhili na wawekezaji.

e) Sekta ya Mawasiliano

68. *Mheshimiwa Spika*, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kupunguza gharama za malipo ya simu za kimataifa ndani ya Jumuiya na zimekubaliana kuwa viwango vya gharama viwe ni Dola za Marekani 0.07 kwa dakika kwa watoa huduma; Dola za Marekaini 0.1 kwa dakika kwa watumiaji wa simu wa kawaida; na kuondoa gharama kwa mpokeaji wa simu iliyounganishwa mionganoni mwa

Nchi Wanachama. Viwango hivi vitaanza kutekelezwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2015/2016.

f) Sekta ya Bandari na Usafiri wa Majini

69. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/15, Wizara imeratibu ukamilishwaji wa zoezi la kukusanya Taarifa za Awali za Hali ya Usafiri wa Majini na Sekta ya Bandari. Taarifa hiyo itatumika katika kuandaa Mkakati wa Usafiri wa Majini wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao pamoja na mambo mengine utaimarisha usalama katika usafiri wa majini baina ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua zote hizi zitawezesha Tanzania kunufaika na fursa iliyonayo ya kijiografia.

g) Miradi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

70. *Mheshimiwa Spika*, mwaka 2011 Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki waliidhinisha miradi ya kipaumbele kwenye Mkakati wa Uchukuzi na Programu ya Maendeleo ya Barabara. Katika Mkakati huo miradi ya ujenzi wa Bandari ya Maruhubi na Chelezo (*dry dock*) na kivuko (*roll on roll off*) imejumuishwa. Nchi Wanachama

zinatakiwa kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi hii yenye sura ya kikanda.

h) Miradi ya Kipaumbele ya Jumuiya ya Uendelezaji wa Miundombinu

71. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Tatu (3) wa Kazi wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Maendeleo ya Miradi ya Miundombinu, uliofanyika mwezi Novemba, 2014, Nairobi, Kenya. Mkutano huo ulipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi 72 ya kipaumbele ya miundombinu (reli, barabara, bandari na nishati) iliyoidhinishwa kwa utekelezaji mwaka 2012. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa asilimia 27 ya miradi iliyoidhinishwa ilikuwa katika hatua za mwanzo za utekelezaji, asilimia 12 ipo katika upembusi yakinifu; asilimia 19 ipo katika upembusi wa kina; asilimia 15 ipo katika hatua ya kutafutiwa fedha; asilimia 12 ipo kwenye mchakato wa zabuni ya Wakandarasi; asilimia 10 ipo katika hatua za ujenzi/utekelezaji; na asilimia 5 imekamilika.

72. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Tanzania miradi iliyokamilika ni pamoja na mradi wa kuupatia umeme mji wa Kibondo mkoani Kigoma; na mradi wa umeme wa msongo wa 132kV unaotoka Ubungo-Ras Kiromoni hadi

Zanzibar (*132kV Ubungo-Ras Kiromoni- Zanzibar Second submarine Interconnector Project*) na barabara ya Tabata – Kinyerezi ambayo ni sehemu ya mradi wa barabara zenyе lengo la kupunguza msongamano katika bandari ya Dar es Salaam. Aidha, ujenzi unaendelea katika barabara za Mbezi Shule – Tangibovu na makutano ya Nelson – Mandela; na barabara ya Nyanguge – Musoma – Sirari, sehemu ya Simiyu – Musoma inayounganisha Tanzania na Kenya.

73. *Mheshimiwa Spika*, katika mkutano huo, Wakuu wa Nchi waliidhinisha Mkakati wa Miaka 10 wa Utekelezaji wa Miradi ya Kipaumbele ya Jumuiya unaobainisha mahitaji ya Dola za Marekani bilioni 100 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyoidhinishwa katika kipindi cha miaka 10 ijayo. Wakuu wa Nchi wameliajiza Baraza la Mawaziri la Jumuiya kuongeza kasi ya utekelezaji wa Miradi hiyo na kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mkakati ulioidhinishwa katika Mkutano ujao wa Nne (4) wa Kazi wa Wakuu wa Nchi kuhusu uendelezaji wa miundombinu unaotarajiwaa kufanyika mwezi Novemba, 2016. Aidha, Wakuu wa Nchi waliidhinisha Mkakati wa Kufungamanisha Sekta za Uchukuzi katika Afrika Mashariki (*Intermodal Transport Strategy in East Africa*) na Mpango wake wa Utekelezaji. Mkakati huo umejikita katika maeneo matatu ambayo ni kuimarishe na kuwianisha sera na mifumo ya

kisheria inayoongoza sekta za uchukuzi zilizofungamanishwa; kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa sekta ya uchukuzi; na kuhuisha miundombinu.

“Ni lazima tutumie nguvu zetu zote kadri tuwezavyo na kwa muda mfupi, kupunguza gharama zinazohusiana na miundombinu. Gharama hizi zinachangia kwa kiasi kikubwa Ukanda wetu kuwa wa gharama kubwa ya kufanya biashara. Inakadiriwa kuwa gharama za usafirishaji katika ukanda wetu ni mara Nne hadi Tano ikilinganishwa na za Nchi zilizoendelea”.

Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki akihutubia Bunge la Afrika Mashariki tarehe 19 Machi, 2015.

3.6 USHIRIKIANO KATIKA SEKTA ZA HUDUMA ZA JAMII

3.6.1 Sekta ya Afya

74. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi ya Sekta ya Afya kama ifuatavyo:

a) Sera na Itifaki ya Afya ya Jumuiya

75. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuratibu majadiliano ya uandaaji wa Sera ya Afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la Sera hii ni kutoa mwongozo katika kutekeleza masuala yote yanayohusu ushirikiano katika sekta ya afya katika Jumuiya. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu ukamilishaji wa Itifaki ya Afya ya Jumuiya, kuwianisha sera, sheria na taratibu za usajili wa madawa ya msingi kwa binadamu kwa kuzingatia viwango vya ubora ndani ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Majadiliano hayo yanatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2015/2016.

b) Mkutano wa Jukwaa la Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

76. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeratibu ushiriki wa wabunge ambao ni wajumbe wa kamati zinazohusika na masuala ya afya katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakiishi, Zanzibar katika mkutano wa saba wa Jukwaa la Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Afya, Idadi ya Watu na Maendeleo uliofanyika mwezi Novemba, 2014 Nairobi, Kenya. Lengo la Jukwaa hili ni kutathmini utekelezaji wa vipaumbele

vilivyokubaliwa katika maeneo ya matumizi ya rasilimali, kuchochaea uwajibikaji wenyе kuleta matokeo; usalama katika afya ya uzazi; na kujadili jinsi ya kuchochaea upatikanaji wa huduma za afya kwa urahisi ili kuwa na huduma endelevu kwa afya ya mama na mtoto. Washiriki wa Jukwaa hili ni Wabunge na Wataalam wa Afya kutoka Nchi Wanachama. Katika Jukwaa la saba, Tanzania iliwakilishwa na Wabunge watano (5); Watatu kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano na wawili kutoka Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

77. *Mheshimiwa Spika*, mkutano huo pamoja na mambo mengine uliazimia kutokutoza kodi vifaa muhimu kwa matumizi ya kuokoa uhai wa binadamu, kuwa na utaratibu wa pamoja wa Jumuiya wa kuboresha uzalishaji wa ndani na ununuzi wa dawa na vifaa vingine muhimu kwa matibabu. Aidha, iliazimiwa mkutano wa nane wa Jukwaa la Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki utafanyika mwezi Oktoba 2015, Dodoma, Tanzania kwa lengo la kutathmini utekelezaji wa Malengo ya Milenia Namba Nne na Tano na kujadili malengo mapya baada ya ukomo wa malengo ya sasa yanayoishia 2015.

78. *Mheshimiwa Spika*, aidha, katika kipindi hiki, ilifanyika Semina ya Nane ya Mabunge ya Nchi Wanachama na Bunge la Afrika Mashariki (*Nanyuki Series VIII*). Semina hiyo

iliyofanyika jijini Kigali, Rwanda ilijadili na kuazimia masuala mbalimbali ya namna ya kukabiliana na changamoto za kiusalamu zinazoikabili Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoa na ugaidi.

c) Kuridhiwa kwa Itifaki ya Kamisheni ya Utafiti wa Afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

79. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Tanzania iliridhia Itifaki ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Utafiti wa Afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na taratibu za kuanzisha Kamisheni hiyo ambayo makao makuu yake yatakuwa Bujumbura, Burundi zimeanza. Usaili umefanyika katika kada ya uongozi ili waanze kuandaa Mipango na Mikakati ya Uendeshaji wa Kamisheni.

3.6.2 Sekta ya Elimu, Utamaduni na Michezo

a. Kuwianisha Mifumo ya Elimu

80. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua ya kuwianisha mifumo ya elimu na mitaala katika Jumuiya ya Afrika Mashariki Kamati ya Wataalam ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imekamilisha taarifa ya utafiti wa namna ya kuwianisha mifumo

ya elimu na mitaala katika Jumuiya. Kwa sasa Nchi Wanachama zinakusanya maoni ya wadau juu ya namna ya kuwianisha mifumo ya elimu na mitaala.

b. Shindano la Insha la Jumuiya

81. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliratibu shindano la uandishi wa Insha la Jumuiya ya Afrika Mashariki linaloshirikisha wanafunzi wa shule za sekondari katika Nchi Wanachama. Washindi wa shindano la mwaka 2014 walikabidhiwa zawadi zao katika Mkutano wa 16 wa Wakuu wa Nchi Wanachama uliofanyika mwezi Februari, 2015. Kwa upande wa Tanzania mwanafunzi Regina Nyamicho kutoka shule ya Sekondari ya Hekima Wilaya ya Bukoba Mjini alishika nafasi ya tatu katika shindano hilo. Aidha, swali la shindano hilo katika mwaka 2015 ni: *Jadili umuhimu wa utulivu wa kisiasa katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Why is political stability important for the integration of the East African Community Partner States?).*

82. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha wanafunzi katika shule za Sekondari zilizopo katika Majimbo yenu kushiriki katika mashindano haya yenye kulenga kuwapa wanafunzi uelewa wa

masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

c. Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki

83. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya Mkataba wa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo majadiliano yanatarajiwu kukamilika mwaka 2015/2016. Aidha, usaili umefanyika kwa watumishi wa nafasi za uongozi wa juu wa Taasisi hii ili waandae Mipango na Mikakati ya Undeshaji wa Kamisheni.

d. Tamasha la *Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni Festival (JAMAFEST)*

84. *Mheshimiwa Spika*, tamasha la JAMAFEST linalenga kuimarisha umoja; ushirikiano, amani na upendo pamoja na kudumisha mila, desturi na tamaduni za Wana Afrika Mashariki. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana, na Michezo imeratibu na kushiriki katika maandalizi ya tamasha hili litakalofanyika mwezi Agosti, 2015 Nchini Kenya. Maandalizi hayo yanahu su kuratibu

na kuhamasisha vikundi vyatyanii na sanaa, ngoma, pamoja na wajasiriamali kushiriki kikamilifu katika Tamasha hilo.

3.6.3 Mradi wa Hifadhi ya Mazingira Katika Bonde la Ziwa Victoria Awamu ya Pili

85. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na uratibu wa majadiliano ya utekelezaji wa shughuli za Mradi wa Hifadhi ya Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria Awamu ya Pili (*Lake Victoria Environmental Management Programme-LVEMP II*) ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Miradi midogo midogo ya kijamii. Hadi kufikia mwezi Novemba, 2014 jumla ya miradi ya kijamii 341 imeendelea kutekelezwa katika eneo la Bonde la Ziwa Victoria. Aidha, majadiliano yanaendelea kati ya Benki ya Dunia na Jumuia kuhusu kuongezewa muda wa miaka miwili na nusu kuanzia mwezi Julai, 2015 ili kuwezesha kukamilika kwa kazi za mradi ambazo hazikukamilika katika Awamu ya Pili na kuandaa Awamu ya Tatu ya Mradi huu (*LVEMP III*).

86. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilifanya ziara ya kukagua na kutathmini utekelezaji wa miradi 14 inayotekelzwa chini ya LVEMP II katika wilaya za Bariadi, Itilima, Maswa, Bunda na Mwanza mjini.

Miradi hiyo inahusu hifadhi ya mazingira katika maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria pamoja na shughuli mbadala za kuwaongeza kipato wananchi wa maeneo hayo na kuachana na shughuli zilizokuwa zikileta uharibifu wa Mazingira katika Ziwa Victoria.

3.6.4 Sekta ya Jinsia na Maendeleo ya Jamii

87. *Mheshimiwa Spika*, katika kuwatambua na kuwashirikisha watu wenye mahitaji maalum katika mtangamano wa Afrika Mashariki, Nchi Wanachama zimekubaliana kuwa na Sera ya Afrika Mashariki ya Watu Wenye Mahitaji Maalum. Maandalizi ya Sera hiyo pamoja na Sera ya Watoto ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanatarajiwu kuanza mwaka 2015/2016.

3.7 USHIRIKIANO KATIKA SIASA, ULINZI NA USALAMA

88. *Mheshimiwa Spika*, Ibara ya 123, 124 na 125 za Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unazitaka Nchi Wanachama kushirikiana katika masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama. Katika mwaka 2014/2015 masuala mbalimbali yalitekelezwa katika maeneo haya kama ifuatavyo:

3.7.1 Masuala ya Siasa

89. *Mheshimiwa Spika*, Ibara ya 127(4) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inamtaka Katibu Mkuu wa Jumuiya kufanya Kongamano linalohusisha sekta binafsi, asasi za kiraia na makundi mengine katika jamii pamoja na Taasisi za Jumuiya. Kongamano hilo hufanyika mara moja kwa mwaka na hutoa fursa kwa makundi hayo kukutana na Katibu Mkuu wa Jumuiya ili kujadiliana masuala mbalimbali kuhusu uendelezaji wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na mapendekezo yanayotolewa huwasilishwa katika Baraza la Mawaziri la Jumuiya kwa majadiliano na utekelezaji.

90. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki kulifanyika Kongamano la tatu lililokuwa na kauli mbiu ya *EAC My Home, My Business*. Mapendekezo yaliyotolewa katika Kongamano hilo ni pamoja na kuongeza kasi ya kurahisisha biashara kati ya Nchi Wanachama za Afrika Mashariki, kuibua njia mbalimbali za kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi, kuhimiza uzalishaji wa chakula cha kutosha, na ushiriki wa sekta binafsi na asasi za kiraia kwenye masuala ya demokrasia na utawala bora.

91. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Tano la mwaka la Utawala Bora la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika mwezi Novemba, 2014 lililokuwa na Kauli mbiu “*Delivering Peaceful and Credible Election for Sustainable Regional Integration – The Role of Key Stakeholders*”. Kongamano hili lilijadili na kutoa mapendekozo juu ya mchango wa vijana, Asasi za kiraia, sekta ya habari, mahakama, vyombo vyta ulinzi na usalama na vyama vyta siasa katika kusaidia uchaguzi kuwa huru na haki katika Nchi Wanachama.

3.7.2 Masuala ya Ulinzi na Usalama

a. Mkakati wa Kikanda wa Kusimamia Amani na Usalama

92. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua ya kukabiliana na changamoto za kiusalama zinazojitokeza katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ilikamilisha mapitio ya Mkakati wa Kikanda wa Amani na Usalama wa mwaka 2006. Mapitio hayo yamehusisha kuongeza maeneo saba (7) katika Mkakati husika. Maeneo hayo ni: uharamia na usalama wa majini; biashara haramu ya usafirishaji binadamu; utakatishaji wa fedha haramu; mauaji ya kimbari na itikadi zake; uhalifu wa kintandao; wizi wa magari na uhalifu dhidi ya mazingira. Mkutano wa

30 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya uliidhinisha Mkakati huo mwezi Novemba, 2014.

b. Kongamano la Viongozi wa Dini

93. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kongamano la viongozi wa dini kutoka Nchi Wanachama lililofanyika mwezi Septemba, 2014. Lengo la kongamano hilo lilikuwa ni kujenga uelewa wa pamoja na kuhimiza ushiriki wa viongozi wa dini katika kudumisha amani na usalama ndani ya Jumuiya. Kongamano hilo liliazimia kushirikiana katika kushughulikia changamoto za kiusalama zinazotokana na uchochezi wa kidini kwa dini zote.

c. Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Tahadhari ya Majanga

94. *Mheshimiwa Spika*, Nchi Wanachama zinatakiwa kuanzisha vituo vyta kitaifa vyta tahadhari ya majanga vyta kuratibu na kutoa taarifa katika kituo cha Kikanda kilichopo Arusha. Katika Mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki katika tathmini ya utayari wa Tanzania kuanzisha Kituo cha Taifa cha Tahadhari ya Majanga. Zoezi hili lilifanyika mwezi Julai, 2014 likihuisha taasisi zote zinazoshughulikia majanga nchini ikiwemo Ofisi

ya Waziri Mkuu, Idara ya Maafa Mamlaka na Hali ya Hewa Tanzania Bara na Zanzibar.

d. Michezo ya Majeshi ya Afrika ya Mashariki

95. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu maandalizi na ushiriki wa Tanzania katika wiki ya Michezo na Utamaduni ya Majeshi kutoka katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika Zanzibar mwezi Agosti, 2014. Lengo la michezo hii ni kuimarisha urafiki, ushirikiano na kuaminiana mionganini mwa askari wa ngazi zote katika majeshi ya Nchi Wanachama.

e. Mfumo wa Kiutendaji wa Jopo la Watu Mashuhuri

96. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika kukamilisha majadiliano ya uanzishwaji wa Jopo la Watu Mashuhuri (*Panel of Eminent Persons*) la Jumuiya ya Afrika Mashariki litakalokwa na jukumu la kusuluhisha migogoro kwa njia ya amani pale itakapojitokeza baina ya Nchi Wanachama au Nchi Mwanachama na Nchi jirani. Utaratibu huu wa kushughulikia migogoro katika Jumuiya uliidhinishwa na Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wao wa 16 uliofanyika mwezi Februari, 2015. Wajumbe wa

kuunda Jopo hilo wanateuliwa kulingana na mahitaji yanavyojitokeza.

f. Kupandisha Hadhi Hati ya Kusafiria ya Afrika Mashariki

97. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Novemba, 2013 Wakuu wa Nchi Wanachama walielekeza Nchi Wanachama kukamilisha majadiliano ya kuipandisha hadhi Hati ya Kusafiria ya Afrika Mashariki kuwa ya Kimataifa ifikapo mwezi Novemba, 2015. Katika kipindi hiki Nchi Wanachama zimekubaliana aina ya muundo (*sample*) wa Hati ya kusafiria itakayotumika kimataifa. Aidha, Nchi wanachama zipo katika hatua mbalimbali za kuboresha mifumo ya uhamiaji na kuweka miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kuanza kutoa Hati hizo. Vilevile, Nchi Wanachama zimekubaliana kuwa uzinduzi wa Hati hizo utafanywa na Wakuu wa Nchi Wanachama katika Mkutano wao unaotarajiwa kufanyika mwezi Novemba, 2015.

98. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa matumizi ya Hati ya Kusafiria ya Afrika Mashariki utategemea kukamilika kwa majadiliano ya Mfumo wa Kielektroniki wa Uhamiaji (*e-Immigration Framework*) wa Afrika Mashariki ambao utaziwezesha Nchi Wanachama kubadilishana habari za kiuhamiaji mionganii

mwao. Majadiliano hayo yanatarajiwa kukamilika na kuwasilishwa katika Kikao cha 32 cha Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Novemba, 2015.

g. Mradi wa Kikanda wa Kusimamia na Kupambana na Uharamia katika Bahari ya Hindi

99. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika ziara ya mafunzo kwa maofisa wa Jeshi la Magereza iliyoandaliwa na Mradi wa Kikanda wa Kupambana na Uharamia katika Bahari ya Hindi. Ziara hiyo ililenga kuwawezesha maafisa magereza kupata uzoefu na kujifunza kutoka nchi nyingine namna ya kuwahifadhi watuhumiwa na wafungwa wa uharamia watakaokamatwa katika Bahari ya Hindi. Hatua hii ni utekelezaji wa Mkakati wa Kikanda wa Kupambana na Uharamia katika Bahari ya Hindi unaojumuisha kanda za SADC, COMESA, IGAD na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkakati huo unatoa majukumu kwa kila kanda ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki imepewa jukumu la kuhifadhi watuhumiwa wa uharamia watakaokamatwa, kuendesha mashtaka dhidi yao, kuwafunga watakaopatikana na hatia na kuwarudisha katika nchi zao mara baada ya kutumikia vifungo vyao.

h. Mapambano Dhidi ya Ugaidi

100. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliratibu na kushiriki katika mikutano ya tathmini ya utayari wa Nchi Wanachama kukabiliana na mtandao wa kimataifa wa uhalifu (*Transnational Organized Crime*) ikiwa ni pamoja na Ugaidi. Lengo la mikutano hiyo lilikuwa ni kupata usoefu na kuainisha changamoto zilizopo katika utendaji, utaaliam na teknolojia inayotumika katika kupambana na mtandao wa kimataifa wa uhalifu na kutoa mapendelekezo ya hatua gani zichukuliwe. Wataalam walipendekeza Nchi Wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki ziimarishe taasisi za kitaifa za kupambana na ugaidi na kuwezesha kubadilishana taarifa ili kuzuia matukio ya kigaidi.

i. Mazoezi ya Pamoja ya Medani ya Kijeshi ‘FTX Ushirikiano Imara, 2014’

101. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika mazoezi ya pamoja ya medani ya kijeshi kwa majeshi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika ngazi mbalimbali yajulikanayo kama FTX (*Field Training Exercise*) Ushirikiano Imara, 2014' yaliyofanyika mwezi Oktoba, 2014 nchini Burundi.

Dhima ya mazoezi hayo kwa mwaka 2014 ilikuwa kujiimarisha katika kukabiliana na ugaidi, uharamia, majanga na operesheni za kurejesha amani. Aidha, Wizara iliratibu na kushiriki katika maandalizi ya awali ya mazoezi ya pamoja ya kijeshi ya vituo vya kamandi kwa Majeshi ya Nchi Wanachama yajulikanayo kama ‘CPX-Ushirikiano Imara 2015” yanayotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2015 nchini Kenya.

3.8 BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

102. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika vikao vitano (5) vya Bunge la Afrika Mashariki ambapo Miswada ya Sheria na Maazimio mbalimbali yalijadiliwa na kupitishwa kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na 6**.

103. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Bunge la Afrika Mashariki lilimchagua Mhe. Daniel Fred Kidega kutoka Jamhuri ya Uganda kuwa Spika wa nne wa Bunge la Afrika Mashariki kufuatia kuondolewa kwa Spika wa tatu Mhe. Margaret Nantongo Zziwa kwa kura za kutokuwa na imani naye. Aidha, katika mkutano wa Kwanza wa Awamu ya Tatu ya Bunge la Tatu la Afrika Mashariki uliofanyika jijini Dar es Salaam, tarehe 24 Agosti – 5 Septemba, 2014 Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki walitembelea Taasisi ya Sanaa

na Utamaduni Bagamoyo ambapo pamoja na mambo mengine, walipanda miti katika taasisi hiyo kama sehemu ya kuendeleza kampeni ya upandaji miti ili kuhifadhi mazingira.

104. *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu iliratibu ziara za Kamati za Bunge la Afrika Mashariki hapa nchini. Kamati hizo ni Kamati ya Mawasiliano, Biashara na Uwekezaji iliyotembelea Mamlaka ya Mapato Tanzania, Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Tanga kwa lengo la kufuatilia hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha. Aidha, kamati mbalimbali za Bunge la Afrika Mashariki zilifanya mikutano ya kukusanya maoni ya wadau kuhusu utungwaji wa sheria mbalimbali za Jumuiya. Kamati hizo ni Kamati ya Kilimo, Maliasili na Mazingira kuhusu Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Afrika Mashariki (*EAC Cooperatives Societies Bill, 2014*); Kamati ya Sheria, Kanuni na Hadhi kuhusu Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Huduma za Kisheria Katika Nchi Wanachama wa Mwaka 2014 (*EAC Cross Border Legal Practice Bill, 2014*); Kamati ya Biashara, Mawasiliano na Uwekezaji, kuhusu Muswada wa Sheria ya Ubunifu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Creative and Cultural Industries Bill, 2015*); na Muswada wa Sheria ya Jumuiya kuhusu Malipo ya Kimtandao (*EAC Electronic Transaction Bill, 2014*).

105. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/15 Mahakama ya Afrika Mashariki ilipokea mashauri mapya 31, ambapo Kitengo cha Awali (*First Instance*) kilipokea mashauri 21 na Kitengo cha Rufaa (*Appellate Division*) kilipokea mashauri 10. Aidha, jumla ya mashauri 53 yalisikilizwa katika Kitengo cha Awali na Kitengo cha Rufaa. Orodha ya Mashauri yaliyosikilizwa na kutolewa uamuzi ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na 7.**

106. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya uteuzi wa Majaji wawili kwa ajili ya kujaza nafasi za Majaji Mhe. James Munange Ogoola, Jaji wa Kitengo cha Rufaa kutoka Uganda atakayemaliza muda wa kuitumikia Mahakama mwezi Agosti 2015 na Mhe Jean Bosco Butasi wa Kitengo cha Awali, kutoka Burundi anayemaliza muda wake mwezi Juni 2015. Majaji walioteuliwa ni Mhe. Jaji Geoffrey W.M. Kirbyabwire wa Kitengo cha Rufaa kutoka Uganda na Mhe. Jaji Audace Ngiye wa Kitengo cha Awali kutoka Burundi. Aidha, Wakuu wa Nchi Wanachama wamemteua Mhe. Jaji Monica Mugenyi kuwa Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Afrika Mashariki kuanzia Mwezi Juni, 2015.

3.10 ELIMU KWA UMMA

107. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano kama ifuatavyo:

a) Ziara za Mipakani

108. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilifanya ziara za kutoa elimu kwa umma kupitia mikutano ya hadhara katika mipaka ya Namanga, Holili, Tarakea, Horohoro, Kabanga, Rusumo, Mutukula na Sirari. Katika ziara hizo, Wizara ilikutana na Jumuiya za wafanyabiashara, watendaji katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya katika mikoa ya Mara, Kilimanjaro, Mwanza, Arusha, Tanga na Kagera. Aidha, ziara hizo zilihusisha watendaji kutoka Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogovidogo; Jumuiya ya Wazalishaji wa Mazao ya Mbogamboga Tanzania (Mkoa wa Arusha); Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo kutoka mikoa yote; Shirikisho la Wenye Viwanda na Chama cha Mawakala wa Utoaji Mizigo Bandarini.

109. *Mheshimiwa Spika*, katika ziara hizo, Wizara ilitoa elimu kwa wadau kuhusu fursa zilizopo katika Jumuiya na kupokea changamoto zinazowakabili wananchi katika kuzitumia fursa hizo kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi. Kutohana

na ziara hiyo, Wizara imekubaliana kushirikiana na sekta binafsi katika kubadilishana taarifa mbalimbali ili kurahisisha uondoaji wa changamoto na kuwezesha wadau kuelewa masuala yanayohusu mtangamano wa Afrika Mashariki. Katika ziara hizo jumla ya machapisho 11,920 yenye ujumbe na taratibu mbalimbali kuhusu masuala ya Afrika Mashariki yalisambazwa kwa wananchi.

b) Vipindi vya Televisheni

110. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu na kushiriki katika kuandaa na kurusha vipindi mbalimbali vya televisheni vyenye lengo la kuelimisha umma juu ya masuala ya mtangamano. Vipindi hivyo ni pamoja na vikao vya Bunge la Afrika Mashariki lililofanyika Dar es Salaam tarehe 27 Agosti – 4 Septemba, 2014 kupitia Televisheni ya TBC1; maonesho ya 38 ya Kimataifa ya Sabasaba kupitia Televisheni za TBC1, Star TV, Clouds TV na CTN; Tamasha la Biashara la Zanzibar kupitia Televisheni ya ZBC.

c) Vipindi vya Redio

111. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwezi Julai, 2014 hadi Februari, 2015 Wizara iliratibu na kushiriki katika kurusha hewani vipindi 19 vya redio kupitia TBC Taifa na Radio

One Stereo. Katika vipindi hivyo, viongozi wa Wizara walishiriki katika majadiliano mbalimbali pamoja na kutoa ufanuzi kwa maswali yaliyokuwa yakiulizwa na wananchi.

d) Machapisho

112. *Mheshimiwa Spika,* Wizara iliandaa nakala 41,500 za machapisho mbalimbali yanayotoa elimu kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, fursa zilizopo na taratibu za kufuatwa ili kunufaika na fursa hizo. Machapisho yalihusu Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Vituo vya Utoaji wa Huduma za Pamoja Mipakani; Miradi ya hifadhi ya Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria; Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Ijue Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Maswali yanayoulizwa mara kwa mara na Wananchi kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, taratibu za kufuata wakati wa kununua au kuuza ndani ya soko la Afrika Mashariki na Kalenda ya Wizara yenye ujumbe maalum kwa wajasiriamali. Machapisho hayo yalisambazwa kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara, Ofisi za Mikoa, Halmashauri, Taasisi Zisizo za Kiserikali na kwa wananchi kupitia mikutano, semina, maonesho, n.k.

e) Maonesho Mbalimbali

113. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki, Wizara ilishiriki katika maonesho ya Kimataifa ya Sabasaba yaliyofanyika, Dar es salaam, Jua Kali/Nguvu Kazi yaliyofanyika Kigali, Rwanda, Tamasha la Biashara lililofanyika Zanzibar na Siku ya Wanawake Duniani. Katika maonesho hayo Wizara ilitoa elimu juu mtangamano wa Afrika Mashariki na kusambaza vipeperushi, majarida na vitabu mbalimbali kuhusiana na Jumuiya kwa lengo la kuelimisha umma. Jumla ya machapisho 5,352 yalisambazwa na jumla ya wananchi 1,338 walitembelea banda la Afrika Mashariki na kupata ufanuzi wa masuala mbalimbali kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zake.

f) Semina

114. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliandaa semina nne za wadau kutoka Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na Vyama vya Kiraia. Aidha, Wizara iliendesha semina ya waandishi wa Habari Zanzibar ambayo ilihusisha vyombo vya habari na waandishi wa vyombo mbalimbali vya Habari vya Zanzibar. Semina hizo pamoja na mambo mengine, zilitoa elimu kuhusu Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Ushirikiano katika masuala ya miundombinu ya

Kiuchumi na Kijamii, Siasa, Ulinzi na Usalama, Umoja wa Forodha, Himaya moja ya Forodha, Umoja wa Fedha na fursa za kiuchumi zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Machapisho mbalimbali kuhusu Jumuiya yalitolewa kwa washiriki wa semina hizo.

g) Mikutano na Waandishi wa Habari

115. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilianda mikutano na Waandishi wa Habari kutoka vyombo mbalimbali iliyotoa taarifa kwa umma kuhusu kufanyika kwa Mkutano wa 30 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya na Mkutano wa 16 wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama; Ufanuzi wa magari ya Tanzania kuzuiliwa kuingia uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta kuchukuwa watalii, Uzinduzi wa Mfumo wa Mawasiliano kwa Njia ya Video (*Video Conferencing System*) ya Wizara na ziara ya kikazi ya Mhe. Rais wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Tanzania. Aidha, waandishi wa habari walijulishwa juu ya Tanzania kukabidhiwa Uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzia Novemba, 2014 hadi Novemba, 2015.

h) Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

116. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu na kushiriki katika uunganishaji na uwekiwa wa

Mfumo wa Mawasiliano kwa Njia ya Video kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Video Conferencing System*). Mfumo huu ambao ulizinduliwa na Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama mwezi Februari, 2015 Nairobi, Kenya. Mfumo huo unatarajiwa kurahisisha mawasiliano na kupunguza gharama za ushiriki kwa baadhi ya vikao visivyo vya maamuzi.

3.11 KUIMARISHA UWEZO WA WIZARA KIUTENDAJI

a. Ajira na Kupandishwa Vyeo kwa Watumishi

117. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara ilipata vibali vya Ajira mpya na mbadala ili kujaza nafasi 42 zilizokuwa wazi. Kati ya nafasi hizo, nafasi 35 za kada mbalimbali zimejazwa kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na 8.**

118. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Wizara iliidhinishiwa nafasi 14 za kuwapandisha vyeo watumishi na nafasi moja ya kumbadilisha kada mtumishi. Aidha, Wizara iliwathibitisha kazini watumishi sita na kuwathibitisha katika vyeo watumishi wanane katika kipindi husika. Hii ni utekelezaji wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma.

b. Mafunzo kwa Watumishi

119. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliandaampango mdogo wa mafunzo kwa mwaka 2014/2015 ambao utekelezaji wake umewezesha watumishi 18 kuhuduria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Kati ya watumishi hao, watumishi 11 wamehuduria mafunzo ya muda mfupi na watumishi saba wanahuduria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Mafunzo ya muda mfupi yaliyotolewa yalihusu Maadili katika Utumishi wa Umma; Usalama Serikalini; Taaluma ya Majadiliano; Uchambuzi wa Sera; na Diplomasia ya Kiuchumi na Uongozi.

c. Ushiriki wa Watumishi katika Michezo ya SHIMIWI

120. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha afya za watumishi, ushirikiano na mshikamano mionganoni mwa Watumishi wa Umma, Wizara iliwezesha watumishi 22 kushiriki katika michezo ya SHIMIWI iliyofanyika mkoani Morogoro kuanzia tarehe 27 Septemba hadi 11 Oktoba, 2014. Katika michezo hiyo Wizara ilipata Kombe la Nidhamu.

**d. Ushirikishwaji wa Watumishi Katika
Utoaji wa Maamuzi**

121. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuwashirikisha Wafanyakazi katika utoaji wa maamuzi kupitia Vikao vya Idara/Vitengo, Vikao Elekezi, Baraza la Wafanyakazi na Mikutano ya Watumishi wote. Aidha, Menejimenti ya Wizara hukutana kila wiki na kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara na jinsi ya kuboresha utendaji na utoaji wa huduma kwa wadau wake.

122. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Wizara ilifanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi ambapo kikao cha kwanza kilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 na kikao cha pili kilijadili na kuidhinisha Bajeti ya wizara kwa mwaka 2015/2016. Pia, Mkataba wa Baraza la Wafanyakazi umepitiwa na kufanyiwa maboresho baada ya kupitwa na wakati na hivyo Baraza la Wafanyakazi kuundwa upya

**e. Mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa
Mteja**

123. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya Mkataba wake wa Huduma kwa Mteja baada ya mkataba uliopo kumalizika muda wake ili uweze

kuendana na wakati na kwa kuzingatia mahitaji na matarajio ya wateja wa Wizara.

3.12 USIMAMIZI WA MAPATO NA MATUMIZI

124. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika Mapato na Matumizi ya fedha za Umma kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za fedha za Umma, Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma na Miongozo mbalimbali ya Serikali. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imefanya vikao vitatu vya Kamati ya Kuratibu, Kusimamia na Kudhibiti Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali.

125. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na usimamizi madhubuti wa Mapato na Matumizi ya fedha za Umma, Wizara yangu imeendelea kupata *Hati Safi* ya ukaguzi wa Hesabu kutoka ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka hadi mwaka. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara yangu ilipata *Hati Safi* isiyio na maeneo ya msisitizo.

4.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

126. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kulijitokeza changamoto mbalimbali katika kipindi hiki kama ifuatavyo:

- a. Kuendelea kupanuka kwa Jumuiya kunakohitaji ongezeko la rasilimali. Wizara itaendelea kujenga hoja Wizara ya Fedha na kuandaa maandiko ya miradi ya maendeleo ikiwa ni hatua ya kukabiliana na changamoto hii;
- b. Vikwazo visivyo vya kiforodha bado vimeendelea kuwa ni changamoto katika utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha hususan katika biashara ya bidhaa baina ya Nchi Wanachama;
- c. Wizara imeendelea kuratibu ubainishaji wa Sheria zinazotakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja linalotoa fursa mbalimbali. Hata hivyo, kumekuwepo na kasi ndogo ya kufanya marekebisho Sheria husika ambapo Wizara imeendelea kuwasiliana na Wizara za Kisekta kuzihimiza kuongeza kasi ya utekelezaji wa suala hili;

- d. Bado wananchi hawajazitumia kikamilifu fursa zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na fursa za kibashara kutokana na uelewa mdogo wa fursa na taratibu. Wizara imeendelea kuelekeza nguvu katika kutoa elimu kwa wafanyabiashara na umma kwa ujumla ikiwa ni hatua ya kukabiliana na changamoto hii;
- e. Kuwepo kwa migogoro katika Bunge la Afrika Mashariki iliyosababisha Bunge hilo kutumia muda mwangi kuipatia ufumbuzi badala ya kushughulikia majukumu yake ya msingi. Hatua zilizochukuliwa na Bunge la Afrika Mashariki katika kukabiliana na changamoto hii ni pamoja na kumchagua Mhe. Daniel Fred Kidega kutoka Jamhuri ya Uganda kuwa Spika wa nne wa Bunge la Afrika Mashariki kufuatia kuondolewa kwa Spika wa tatu Mhe. Margaret Nantongo Zziwa kwa kura za kutokuwa na imani naye.
- f. Kwa kuwa Bunge la Afrika Mashariki ndicho chombo kikuu cha kutunga sheria za Jumuiya na sheria hizo kwa

mujibu wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya zinapewa nguvu juu ya sheria za Nchi Wanachama katika masuala ya utekelezaji wa Mkataba huo; na kwa kuwa wajumbe wa Bunge hilo wanaruhusiwa kimkataba kuwasilisha hoja na miswada binafsi Bungeni kwa majadiliano na maamuzi, fursa ambayo wawakilishi wa baadhi ya nchi wanachama wameitumia kikamilifu kwa maslahi mapana ya nchi zao; na kwa kuwa lugha rasmi ya Jumuiya ni Kiingereza na maamuzi ndani ya Bunge hilo yanatokana na ushawishi wa hoja unaotaka ujuzi wa kutosha wa lugha rasmi ya majadiliano; na kwa kuwa kufikiwa kwa maamuzi ndani ya Bunge hilo ni kwa ushawishi wa hoja na kupigiwa kura, tofauti na utaratibu wa maridhiano (*consensus*) unaotumika na vyombo vingine vya Jumuiya, Wizara inaliomba Bunge hili kwa mara ya pili sasa na kabla hatujaharibikiwa kabisa, libadilishe mapema iwezekanavyo utaratibu dhaifu na mbovu tuliouendekeza kwa muda mrefu wa kupata wawakilishi wa Taifa letu kwenye chombo hiki adhimu ambao hauzingatii kabisa uzito wa majukumu yao, uwezo mkubwa kielimu/kiuelewa

wa wawakilishi wenzao, na ushindani/mvutano mkali wa kimaslahi baina ya Nchi Wanachama unaotaka wawakilishi makini, imara, wazalendo wenyewe ujuzi, uzoefu na weledi mtambuka na umiliki wa kuridhisha wa lugha ya majadiliano Bungeni. Bila maamuzi haya ya makusudi, hatuwezi kukwepa sifa ya kuwa wasindikizaji katika mchakato unaoendelea wa mtangamano ambao umeingia ngazi za ki-weledi zaidi: Himaya Moja ya Forodha, Soko la Pamoja, Umoja wa Fedha; na hatimaye Shirikisho la Kisiasa.

5.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/2016

127. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Wadau mbalimbali, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i. Kuratibu maandalizi na kuongoza majadiliano katika mikutano ya Wakuu wa Nchi Wanachama, Baraza la Mawaziri la Jumuiya, Mabaraza ya Mawaziri ya Kisekta ya Jumuiya, Vikundi Kazi na Wataalam;

- ii. Kuendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya na Baraza la Mawaziri la Jumuiya;
- iii. Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa miaka kumi wa Umoja wa Fedha katika kuelekea kuwa na Sarafu Moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- iv. Kuratibu uridhiwaji wa Itifaki mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizokwishesainiwa na Nchi Wanachama;
- v. Kuendelea na zoezi la mapitio ya Sheria za Tanzania ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki; pamoja na kuratibu utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki;
- vi. Kuendelea kuratibu, kushiriki na kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (*EAC – EU Economic Partnership Agreement*); majadiliano kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani; na

majadiliano ya utatu wa COMESA-EAC-SADC;

- vii. Kuendelea kuratibu na Kufuatilia utekelezaji wa Miradi na Programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na miradi ya uendelezaji wa miundombinu (reli, barabara, bandari, nishati na viwanja vya ndege na hali ya hewa) na maeneo ya ushirikiano katika sekta ya kijamii (elimu, afya, mazingira, jinsia na watoto) ya Jumuiya;
- viii. Kuendelea kuratibu uanzishaji wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja katika Mipaka ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na uandaaji wa Kanuni za kutekeleza Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uendeshaji wa Vituo vya kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani na Sheria ya Jumuiya ya Kudhibiti Uzito wa Magari;
- ix. Kuratibu uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha katika biashara baina ya Nchi Wanachama;
- x. Kuendelea kuratibu ushiriki katika Mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki

- (EALA) na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na mikutano kati ya Wizara na Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki;
- xi. Kuendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano kuhusu Jamhuri za Sudan Kusini na Somalia ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki;
 - xii. Kuendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya utekelezaji wa maeneo ya ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama;
 - xiii. Kuendelea kuratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuipandisha hadhi Pasi ya kusafiria ya Afrika Mashariki kuwa ya Kimataifa na katika majadiliano ya kutoa huduma za Visa na huduma za kibalozi kwa niaba ya Nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;
 - xiv. Kuendelea kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zilizopo kupitia Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara;

- xv. Kuratibu mapitio, utafiti, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mtangamano wa Afrika Mashariki;
- xvi. Kulipa mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- xvii. Kuratibu utekelezaji wa masuala mtambuka yanayohusu Jinsia, Utawala Bora na mapambano dhidi ya UKIMWI;
- xviii. Kuendelea kuratibu utoaji wa huduma za kiutawala na kiutumishi; na
- xix. Kuendelea kuimarisha mifumo ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Mifumo ya Ununuzi pamoja na kuandaa daftari la Kudhibiti na Kusimamia Viashiria Hatarishi (*Risk Register*).

6.0 SHUKRANI

128. *Mheshimiwa Spika*, washirika mbalimbali wa maendeleo wamechangia katika utekelezaji wa shughuli za Jumuiya katika kipindi hiki. Napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wizara na Jumuiya kwa ujumla kuwashukuru na kuwatambua kama ifuatavyo: Serikali za Uingereza, Finland, Norway, Marekani, Ujeruman; Ufaransa, Canada, Sweden, Ubelgiji, Denmark na

Japan. Aidha, natoa shukrani kwa Mashirika na Taasisi za Kimataifa za Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID), Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA), Benki ya Japan ya Maendeleo ya Kimataifa, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Rockefeller Foundation, Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IMO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), Investment Climate Facility for Africa (ICF), Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID), African Capacity Building Facility (ACBF), The Association of European Parliamentarians with Africa (AWEPA) na TradeMark East Africa (TMEA).

7.0 MAOMBI YA FEDHA ZA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016

129. *Mheshimiwa Spika*, ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa katika mwaka 2015/2016, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 24,598,190,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 2,618,968,000 ni Mishahara ya Watumishi na Shilingi 21,979,222,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

130. *Mheshimiwa Spika*, Hotuba hii ina viambatisho mbalimbali. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kuwa ni vielelezo vyta hoja hii.

Aidha, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya www.meac.go.tz.

131. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

Kiambatisho Na. 1: Bidhaa Ambazo Zimeingizwa Katika Mfumo wa Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki Katika Kipindi cha Majaribio

Na.	Nchi Mwanachama	Bidhaa Kutoka Nje ya Jumuiya	Bidhaa Kutoka Ndani ya Jumuiya
1.	Burundi	Ngano na bidhaa zinazoagiz wa na kampuni ya BRARUDI, samani, vipuri vya pikipiki na bidhaa za plastiki.	Saruji, vipodozi, chupa tupu zinazozalishwa na kiwanda cha Kioo Limited na mafuta ya kupikia.
2.	Kenya		Sabuni, sigara na neutral spirits, bidhaa za chuma, mafuta ya kupikia, mahindi, sukari na mchele.
3.	Rwanda	Ngano, mafuta ya petroli, mchele na sukari.	Mchele, sukari, saruji na chumvi.
4.	Uganda	Mafuta ya petrol.	Bidhaa zote zilizolipiwa kodi (duty-paid goods).

Kiambatisho Na.2: Mwenendo wa Biashara ya Jumla (*Mauzo na Manunuzi*), 2007-2013 (US\$ Millioni)

Nchi	Mwaka/Thamani						
	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013
Uganda	675.30	762.0	945.75	1,005.13	1,196.36	1,227.21	1,244.02
Tanzania	279.50	735.8	601.91	690.16	787.14	1,291.90	1,515.00
Kenya	1,018.40	1,218	1,331.97	1,536.80	1,847.23	1,957.29	1,785.50
Burundi	94.99	95.59	101.04	95.79	189.09	193.00	381.57
Rwanda	247.03	337.7	456.63	395.00	466.21	801.29	879.48
Jumla	2,315.2	3,149	3,437.3	3,722.9	4,486	5,470.7	5,805.57

Chanzo: Taarifa ya Biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2013.

Kiambatisho Na. 3: Miradi Iliyowekezwa Hapa Nchini na Nchi Wanachama Mwaka 2014.

Nchi Mwanachama	Sekta	Idadi ya Miradi	Idadi ya Ajira	Thamani ya Mradi (US\$ Mil)
Kenya	Kilimo	1	52	0.29
	Majengo ya Biashara	7	40	6.50
	Taasisi za Fedha	1	1	0.10
	Rasilimali Watu	1	4	0.38
	Uzalishaji Viwandani	13	422	54.92
	Maliasili	1	31	1.10

	Mawasiliano ya Simu	1	4	0.16
	Utalii	2	77	2.74
	Uchukuzi	9	348	17.35
Rwanda	Uchukuzi	1	90	7.20
Uganda	Rasilimali Watu	2	102	7.50
	Uchukuzi	1	61	2.90
Jumla		40	1,233	101.14

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania, 2014

Kiambatisho Na. 4: Mitandao ya Barabara Zinazounganisha Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki

Na.	Kanda	Mitandao ya Barabara
1.	Kaskazini	Mombasa – Voi – Eldoret – Malaba – Bugiri – Kampala – Masaka - Katuna/Gatuna – Kigali – Akanyaru -Kayanza-Bujumbura.
2.	Kati	Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma – Singida – Nzega – Tinde – Isaka - Lusahunga kuelekea: (i) Rubavu kupitia Rusumo na Kigali; (ii) Bujumbura kupitia Nyakasanza, Kabanga/Kobero na Gitega; (iii) Masaka kupitia Bukoba na Mutukula; na (iv) Nyakahura – Murusagamba/Muruma - Cankuzo – Gitega
3.	Ziwa Victoria	Sirari Corridor (Biharamulo - Mwanza- Musoma - Sirari/Isebania - Kisii - Kisumu- Webuye- Kitale - Kapenguria - Makutano – Lodwar.
4.	Ziwa Tanganyika	Sumbawanga Corridor (Tunduma- Sumbawanga-Uvinza – Kidahwe- Mwandiga – Manyovu/Mugina - Mabanda - Nyanza Lac-Rumonge – Bujumbura - Ruhwa – Rusizi – Rubavu.

5.	Namanga	<i>Trans-African Highway No. 8 Corridor</i> (Tunduma - Mbeya - Iringa - Dodoma - Babati - Arusha - Namanga - Nairobi - Thika-Murang'a - Embu- Nyeri - Nanyuki - Isiolo - Marsabit- Moyale yenye michepuko kuelekea: (i) Mbeya - Tukuyu - Kasumulu (Mpaka wa Tanzania na Malawi); na (ii) Iringa - Morogoro
6.	Pwani	<i>Coastal Corridor</i> (Mingoyo - Dar es Salaam - Bagamoyo -Makurunge - Mkwaja-Pangani-Tanga - Horohoro/Lungalunga-Mombasa-Malindi-Lamu.
7.	Mtwara	Mtwara Corridor: Mtwara - Mingoyo - Masasi -Tunduru - Songea - Mbamba Bay yenye michepuko kuelekea Mangaka - Mtambaswala (Mpaka wa Tanzania na Msumbiji).
8.	LAPSSET - Lamu Port South Sudan Ethiopia Corridor	Lamu - Garisa - Isiolo - Lodwar - Nadapal (Mpaka wa Kenya na Sudan Kusini).
9.	Tanga	Tanga - Arusha-Musoma-Kampala (Bukasa, <i>Port Bell</i>).
10.	Gulu	Tororo - Mbale - Soroti- Lira - Gulu - Nimule.

Kiambatisho Na. 5: Hatua Iliyofikiwa Katika Ujenzi wa Vituo Vya Utoaji wa Huduma kwa Pamoja Mipakani (*One Stop Border Posts-OSBPs*)

Na.	Kituo	Hatua ya Ujenzi Iliyofikiwa kwa upande wa Tanzania
1.	Holili/Taveta (Tanzania na Kenya)	Ujenzi umekamilika.
2.	Sirari/Isebania (Tanzania na Kenya)	Ujenzi umekamilika.
3.	Mutukula/Mutukula (Tanzania na Uganda)	Ujenzi umekamilika
4.	Namanga/Namanga (Tanzania na Kenya).	Ujenzi umekamilika
5.	Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi).	Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 85.
6.	Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda)	Ujenzi umekamilika.
7.	Horohoro/Lungalunga, (Tanzania na Kenya).	Ujenzi umekamilika

Kiambatisho Na 6: Miswada ya Sheria Iliyopitishwa, Inayoendelea Kujadiliwa na Maazimio ya Bunge la Afrika Mashariki Katika Mwaka 2014/2015

Na.	Miswada ya Sheria
Miswada ya Sheria Iliyopitishwa	
1.	Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Afrika Mashariki wa Mwaka, 2014 (<i>The East African Community Cooperatives Societies Bill, 2014</i>).
2.	Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza ya Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka, 2015 (<i>The East African Community Supplementary Appropriation Bill, 2015</i>).
3.	Muswada wa Sheria ya kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka, 2015 (<i>The East African Community Elimination of Non-Tariff Barriers Bill, 2015</i>).
4.	Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Umoja wa Forodha wa Mwaka 2015 (<i>The East African Community Customs Management (Amendment) Bill, 2015</i>).
5.	Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Elimu ya Mtangamano wa Afrika Mashariki wa Mwaka, 2014 (<i>The East African Community Integration (Education) Bill, 2014</i>).
Miswada ya Sheria Inayoendelea Kujadiliwa	
1.	Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Umoja wa Forodha wa Mwaka, 2015 (<i>The East African Community Customs Management (Amendment) Bill, 2015</i>).
2.	Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka, 2015 (<i>The East African Community Science and Technology Commission Bill, 2015</i>).

3.	Muswada wa Sheria ya Ubunifu na Biashara ya Masuala ya Kiutamaduni ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka, 2015 (<i>The East African Community Creative and Cultural Industries Bill, 2015</i>).
4.	Muswada wa Sheria ya Biashara Mtandao ya Afrika Mashariki wa Mwaka, 2014 (<i>The East African Community Electronic Transaction Bill, 2014</i>);
5.	Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Misitu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka, 2015 (<i>The East African Community Forest Management & Protection Bill, 2015</i>).
6.	Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Ushindani ya Afrika Mashariki wa Mwaka, 2015 (<i>The East African Community Competition (Amendment) Bill, 2015</i>).

MAAZIMIO

1.	Azimio la Bunge la Kuunda Kamati ya Kushughulikia Mauaji ya Kimbari “A Motion for a Resolution of the Assembly to appoint a Select Committee on Genocide”. Hoja iliwasilishwa na Mhe. Abubakar Ogle wa Kenya.
2.	Azimio la Bunge la Kuanzisha Kituo cha Bunge la Afrika cha Amani na Usalama “A Motion for a Resolution of the Assembly for the Establishment of the African Parliament Centre for Peace and Security (APCPS).
3.	Azimio la Bunge la Kuzitaka Nchi Wanachama za Afrika Mashariki Kuridhia Mkataba wa Afrika Kuhusu Demokrasia, Chaguzi na Utawala “A Motion for a Resolution of the Assembly urging EAC Partner States to adopt the African Charter on Democracy, Elections and Governance.

**Kiambatisho Na 7: Orodha ya Mashauri
Yaliyosikilizwa na Kutolewa Uamuzi katika
Mwaka 2014/2015**

Na.	Kesi
Kesi Zilizofunguliwa Katika Kitengo cha Awali	
1	Application No. 15 of 2014 (Arising from Reference No. 12 of 2014) James Alfred Koroso Vs The Hon. Attorney General of the Republic of Kenya. Filed on 21 st July 2014.
2	Application No. 16 of 2014 (Arising from Reference No. 8 of 2014) The Attorney General of the Republic of Rwanda Vs Union Trade Centre Limited. Filed on 13 th August 2014.
3	Application No. 17 of 2014 (Arising from Reference No. 2 of 2011) Attorney General of the Republic of Uganda Vs The East Africa Law Society and the Secretary General of the East African Community. Filed on 2 nd September, 2013.
4	Application No. 18 of 2014 (Arising from Reference No. 13 of 2014) Mr. Bonaventure & 2 Others Vs the Attorney General of the Republic of Burundi. Filed on 5 th September, 2013.
5	Application No. 19 of 2014 (Arising from Reference No. 10 of 2012) Niyitegeka Theoneste Vs The Attorney General of the Republic of Rwanda. Filed on 16 th October, 2014.
6	Application No. 20 of 2014 (Arising from Reference No. 6 of 2014) UHAI EASHRI Vs Human Rights Awareness & Promotion Forum and the Attorney General of the Republic of Uganda. Filed on 1 st October, 2014.
7	Application No. 21 of 2014 (Arising from Reference No. 6 of 2014) Health Development Initiative-Rwanda Vs Human Rights Awareness & Promotion Forum and the Attorney General of the Republic of Uganda. Filed on 24 th October, 2014.
8	Application No. 22 of 2014 (Arising from Reference No. 2 of 2011) The Attorney General of the Republic of Uganda Vs The East African Law Society and The Secretary General of the East African Community. Filed on 28 th October, 2014.
9	Application No. 23 of 2014 (Arising from Reference No. 17 of 2014) Rt. Hon. Margaret Zziwa Vs The Secretary General of the East African Community. Filed on 10 th December, 2014.

10	Application No. 1 of 2015 (Arising from Reference No. 6 of 2014) Dr. Ally Possi & Another Vs Human Rights Awareness & Promotion Forum 9HRAPF) & The Attorney General of the Republic of Uganda. Filed on 13 th April 2015.
11	Reference No. 10 of 2014 Dr. Mpozayo Christophe Vs The Attorney General of the Republic of Rwanda. Filed on 7 th July, 2014.
12	Reference No. 11 of 2014 Mr. Audace Ngendakumana Vs The Attorney General of the Republic of Burundi and The Secretary General of the East African Community. Filed on 18 th July, 2014.
13	Reference No. 12 of 2014 James Alfred Koroso Vs The Hon. Attorney General of the Government of Kenya and the Permanent Secretary Ministry of State for Provincial Administration and Internal Security. Filed on 21 st July, 2014.
14	Reference No. 13 of 2014 Mr. Bonaventure & 2 Others Vs the Attorney General of the Republic of Burundi. Filed on 29 th August 2014.
15	Reference No. 14 of 2014 Ndagire Lilian Rovince & 2 Others Vs The Attorney General of Uganda. Filed on 6 th November, 2014.
16	Reference No. 15 of 2014 Mr. Baranzira Raphael & Mr Ntakiyiruta Joseph Vs The Attorney General of the Republic of Burundi. Filed on 17 th November 2014.
17	Reference No. 16 of 2014 Ronald Ssembuusi Vs The Attorney General of the Republic of Uganda. Filed on 2 nd December, 2014.
18	Reference No. 17 of 2014 Rt. Hon. Margaret Zziwa Vs The Secretary General of the East African Community. Filed on 10 th December, 2014.
19	Taxation Cause No. 2 of 2014 (Arising from Reference No. 5 of 2013) National Medical Stores Vs Godfrey Magezi. Filed on 12 th September, 2014.
20	Taxation Cause No. 3 of 2014 M/s Semuyaba, Iga Advocates Vs M/s Quality Chemical Industries Limited. Filed on 7 th October, 2014.
21	Taxation Cause No. 1 of 2015 The Inspector General of the Government vs Godfrey Magezi. Filed on 17 th April 2015.

Rufaa na Kesi Zilizopokelewa na Kitengo cha Rufaa	
22	Appeal No. 3 of 2014 The Honorable Attorney General of the United Republic of Tanzania Vs African Network for Animal Welfare. Filed on 4 th September 2014.
23	Appeal No. 4 of 2014 Angella Amudo Vs The Secretary General of the East African Community. Filed on 10 th October, 2014.
24	Appeal No. 5 of 2014 The Attorney General of the Republic of Uganda Vs The East Africa Law Society and the Secretary General of the East African Community. Filed on 4 th November 2014.
25	Case Stated No. 1 of 2014 The Attorney General of the Republic of Uganda and Tom Kahurwenda. Filed on 17 th November, 2014.
26	Appeal No. 6 of 2014 Henry Kyarimpa Vs Attorney General of the Republic of Uganda. Filed on 31 st December, 2014.
27	Appeal No. 1 of 2015 Union Trade Centre Ltd (UTC) VS The Honorable Attorney General of the Republic of Rwanda. Filed on 12 th January 2015.
28	Appeal No. 2 of 2015 The Attorney General of the United Republic of Tanzania vs Anthony Calist Komu. Filed on 22 nd April 2015.
29	Application No. 1 of 2015 The Attorney General of the United Republic of Tanzania vs Anthony Calist Komu. Filed on 26 th February, 2015.
30	Application No. 3 of 2015 Timothy Alvin Kahoho vs the Secretary General of the East African Community. Filed on 3 rd March 2015.
Kesi Zilizosikilizwa na Kitengo cha Awali	
31	Application No. 6 of 2013 (Arising from Reference No. 9 of 2013 Ally Hatibu Msangi & 2 Others Vs The Secretary General of the East African Community & 3 Others. Ruling was delivered on 2 nd September, 2014.
32	Application No. 12 of 2014 (Arising from Reference No. 8 of 2013) Uganda Traders Association of Southern Sudan & 3 Others Vs The Attorney General of Uganda & 4 Others. The Ruling was delivered on 4 th September, 2014.
33	Application No. 14 of 2014 (Arising from Application No. 12 of 2014 arising from Reference No. 8 of 2013) Uganda Traders Association of South Sudan Ltd & 3 Others Vs The

	Attorney General of Uganda & 5 Others. The Ruling was delivered on 4 th September, 2014.
34	Reference No. 5 of 2013 Godfrey Magezi Vs The Attorney General of Uganda and 5 Interested Parties. The judgment was delivered on 14 th May, 2015.
35	Application No. 15 of 2014 (Arising from Reference No. 12 of 2014) James Alfred Koroso Vs The Hon. Attorney General of the Government of Kenya and the Permanent Secretary Ministry of State for Provincial Administration and Internal Security. The Ruling was delivered on 4 th November, 2014.
36	Reference No. 7 of 2013 Burundian Journalists Union Vs The Attorney General of the Republic of Burundi. The judgment was delivered on 15 th May, 2015.
37	Reference No. 1 of 2014 The East Africa Law Society Vs The Attorney General of the Republic of Burundi and the Secretary General of the East African Community. The judgment was delivered on 15 th May, 2015.
38	Application No. 16 of 2014 (Arising from Reference No. 8 of 2014) The Attorney General of the Republic of Rwanda Vs Union Trade Centre Limited. The ruling was given on 22 nd September, 2014.
39	Reference No. 10 of 2012 Mr. Niyitegeka Theoneste Vs The Attorney General of the Republic of Rwanda. The judgment was delivered on 23 rd September, 2014.
40	Reference No. 9 of 2013 Ally Hatibu Msangi & 2 Others Vs The Secretary General of the East African Community & 3 Others. The Reference was heard on 24 th February, 2015.
41	Reference No. 7 of 2014 East Africa Law Society Vs The Secretary General of the Community. Sheduling Conference was held on 5 th November, 2014
42	Reference No. 6 of 2014 Human Rights Awareness & Promotion Forum Vs The Attorney General of the Republic of Uganda. Sheduling Conference was held on 22 nd April, 2015
43	Reference No. 9 of 2014 Oscar Okaly Opuli Vs The Secretary General of the East African Community & The Attorney General of the Republic of Uganda. Sheduling Conference was held on 23 rd February, 2015
44	Application No. 18 of 2014 (Arising from Reference No. 13 of 2014) Mr. Bonaventure Gasutwa Vs The Attorney General of the Republic of Burundi. The ruling was delivered on 28 th November, 2014.
45	Reference No. 2 of 2014 UPRONA Party & 2 Others Vs The Attorney General of the Republic of Burundi and The

	Secretary General of the East African Community. Scheduling Conference was held on 13 th November, 2014
46	Reference No. 4 of 2014 Mr. Georges RUHARA Vs The Attorney General of the Republic of Burundi and the Secretary General of the East African Community. Hearing was on 29 th April, 2015
47	Reference No. 10 of 2014 Dr. Mpozayo Christophe Vs The Attorney General of the Republic of Rwanda. Scheduling Conference was held on 18 th November, 2014
48	Application No. 23 of 2014 (Arising from Reference No. 17 of 2014) Rt. Hon. Dr. Margaret Zziwa Vs The Secretary General of the East African Community. The ruling was delivered on 3 rd February, 2015
49	Application No. 19 of 2014 (Arising from Reference No. 10 of 2012) Niyitegeka Theoneste Vs The Attorney General of the Republic of Rwanda. The application was heard on 3 rd February, 2015
50	Application No. 20 of 2014 (Arising from Reference No. 6 of 2014) UHAI EASHRI Vs Human Rights Awareness & Promotion Forum and the Attorney General of the Republic of Uganda. The ruling was delivered on 17 th February, 2015.
51	Application No. 21 of 2014 (Arising from Reference No. 6 of 2014) Health Development Initiative- Rwanda Vs Human Rights Awareness & Promotion Forum and The Attorney General of the Republic of Uganda. The ruling was delivered on 17 th February, 2015.
52	Reference No. 12 of 2014 James Alfred Koroso Vs The Attorney General of Kenya & Another. Hearing was on 8 th May, 2015
53	Reference No. 11 of 2014 Audace Ngendakumana Vs The Attorney General of the Republic of Burundi and The Secretary General of the East African Community. The Scheduling Conference was held on 13 th February, 2015
54	Reference No. 13 of 2014 Bonaventure Gasutwa & 2 Others Vs The Attorney General of the Republic of Burundi. Scheduling Conference was held on 13 th February, 2015.
55	Application No. 22 of 2014 (Arising from Reference No. 2 of 2011) The Attorney General of the Republic of Uganda Vs The East Africa Law Society and the Secretary General of the East African Community. The application was heard on 19 th February, 2015
56	Reference No. 17 of 2014 Rt. Hon. Dr. Margaret Zziwa Vs The Secretary General of the East African Community.

	Scheduling Conference was held on 23 rd February, 2015
Hukumu Zilizotolewa na Kitengo cha Awali	
57	Reference No. 7 of 2012 Anthony Calist Komu Vs Attorney General of the United Republic of Tanzania. The judgment was delivered on 26 th September, 2014.
58	Claim No. 1 of 2012 Angella Amudo Vs The Secretary General of the East African Community. The judgment was delivered on 26 th September, 2014.
59	Reference No. 8 of 2013 Uganda Traders Association of South Sudan Ltd. and 3 Others Vs The Attorney General of Uganda and 5 Others Filed on 10 th October 2013. The judgment was delivered on 27 th February, 2015
60	Reference No. 10 of 2013 Union Trade Centre Limited (UTC) Vs The Attorney General of the Republic of Rwanda. The judgment was delivered on 27 th November, 2014
61	Reference No. 4 of 2013 Henry Kyarimpa Vs The Attorney General of the Republic of Uganda. The judgment was delivered on 28 th November, 2014
62	Reference No. 2 of 2013 Benoit Ndorimana Vs The Attorney General of the Republic of Burundi. The judgment was delivered on 26 th September, 2014
Taxations Heard and Rulings Delivered	
63	Taxation No. 1 of 2013 Hon. Sitenda Sebalu Vs The Secretary General of the East African Community. Ruling was delivered on 20 th March, 2015.
64	Taxation No. 1 of 2013 Hon. Sitenda Sebalu Vs The Secretary General of the East African Community. Ruling was delivered on 20 th March, 2015.
65	Electoral Commission vs Hon. Sitenda Sebalu. Ruling was delivered on 20 th March, 2015.
66	Taxation Cause No. 4 of 2013 (Arising from Application No. 3 of 2012) Hon. Sitenda Sebalu Vs The Secretary General of the East African Community. Ruling was delivered on 20 th March, 2015.
67	Taxation Cause No. 5 of 2013 (Arising from Reference No. 6 of 2012) Among Anita Vs Attorney General of Uganda. Ruling was delivered on 20 th March, 2015.
68	Taxation Cause No. 1 of 2014 (Arising from Reference No. 1 of 2010) Hon. Sitenda Sebalu Vs The Secretary General of the East African Community. Ruling was delivered on 20 th

	March, 2015.
Appeal Heard by Appellate Division	
69	Appeal No. 3 of 2014 The Honorable Attorney General of the United Republic of Tanzania Vs African Network for Animal Welfare. The Appeal was heard on 28 th January, 2015.
70	Appeal No. 4 of 2014 Angella Amudo Vs The Secretary General of the East African Community. The hearing was on 13 th April, 2015.
71	Appeal No. 2 of 2013 Timothy Alvin Kahoho Vs The Secretary General of the East African Community. The judgment was delivered on 28 th November, 2014.
72	Appeal No. 3 of 2013 Alcon International Limited Vs. The Standard Chartered Bank of Uganda & 2 Others. The Appeal was heard on 20 th January, 2015.
73	Reference on Taxation No. 1 of 2014 Alcon International Limited Vs. The Standard Chartered Bank of Uganda & 2 Others. The Reference was heard on 22 nd January, 2015.
74	Appeal no. 1 of 2014, Democratic Party Vs. The Secretary General of the East African Community & 4 others. The Appeal was heard on 26 th January, 2015.
75	Appeal No. 3 of 2014, Attorney General of the United Republic of Tanzania Vs. African Network for Animal Welfare (ANAW). The Appeal was heard on 28 th January, 2015.
76	Appeal No. 5 of 2014, Attorney General of the Republic of Uganda Vs. The East Africa Law Society & Another. The judgment was delivered on 16 th April, 2015.
77	Appeal No. 6 of 2014 Henry Kyarimpa vs the Attorney General of the Republic of Uganda. Sheduling conference was held on 20 th April, 2015.
78	Appeal No. 1 of 2015 Union Trade Centre Ltd (UTC) vs The Attorney General of Rwanda. Sheduling conference was held on 22 nd April, 2015.
79	Case Stated No. 1 of 2014 The Attorney General of Uganda vs Tom Kyahurwenda. The case was heard on 24th April, 2015.

**Kiambatisho Na 8: Ajira Mpya na Mbadala kwa
Mwaka 2014/2015**

A. Ajira Mpya		
Na.	Kada	Idadi ya Watumishi
1	Afisa Tawala	5
2	Afisa Utumishi	1
3	Wachumi	11
4	Mtakwimu	1
5	Mhandisi	1
6	Afisa Usimamizi wa Fedha	1
7	Afisa Biashara	1
8	Afisa Maendeleo ya Jamii	1
9	Afisa TEHAMA	2
10	Afisa Habari	1
11	Mkaguzi wa Ndani	1
12	Afisa Sheria	1
13	Msaидizi wa Kumbukumbu	3
14	Katibu Mahsus	3
15	Jumla Ndogo	33

B. Ajira Mbadala		
1	Afisa Usafirishaji	1
2	Msaيدizi wa Kumbukumbu	1
	Jumla Ndogo	2
	Jumla Kuu	35